Kikao cha Saba – Tarehe 18 Oktoba, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha hati mezani juu ya mswada wa sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani juu ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 30

Ushiriki wa Waandishi wa Habari katika Ziara za Viongozi

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny. Mhe. Nassor Salim Ali) – Aliuliza:-

Kwanza nampongeza Mhe. Waziri wa Fedha kwa juhudi yake ya kuwashirikisha waandishi wa habari katika ziara ya mafunzo nchini China kwa Viongozi wa Serikali. Hili linafaa kupongezwa na ni vizuri likawekewa kumbukumbu katika maktaba za vyombo hivyo vya habari, ili siku za mbele zikitakiwa kumbukumbu hizo zipatikane kwa manufaa ya Zanzibar.

(a) Je, ni waandishi wangapi pamoja na majina yao na taasisi wanazotoka wamepata fursa katika kutuma habari kutoka China.

(b) Je, fedha ambazo zimetumika kuwasafirisha waandishi hao zimepatikana wapi, kutoka taasisi zao au Wizara inayohusika na masuala ya Fedha.

(c) Je, utaratibu gani umetumika katika uteuzi wa waandishi hao.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo) – Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mjumbe swali lake Nam. 30 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni wajibu wa serikali kuwashirikisha waandishi katika mambo yote ya utekelezaji kwa lengo la kuifahamisha jamii na si kwenye ziara tu peke yake. Aidha ushauri alioutoa Mhe. Mwakilishi wa kuwekwa kumbukumbu kwa ziara hizi kwa vyombo vya habarui tumeupokea na tunauchukua kwa kuufanyia kazi zaidi. Na ni kweli utaleta manufaa kwa nchi yetu.

Naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Ni waandishi kumi (10) kutoka vyombo mbali mbali vikiwemo *ZBC*, (Televisheni na Radio) *Star TV*, *TBC* ndio waliopata fursa kutuma habari kutoka China.

(b) Fedha zilizotumika kuwasafirishia waandishi hawa ni kutoka Taasisi zao na vile vile kutoka fungu la msaada kwa kuijengea Uwezo Zanzibar iliyotolewa na ndugu zetu wa Jamhuri ya Watu wa China.

(c) Utaratibu uliotumika katika uteuzi wa wanandishi hao ni wa kuorodhesha wale wote wenye juhudi ya kazi, sifa za kujituma na uzoefu wa kutuma habari za Maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwanza niipongeze serikali kwa juhudi zake hizi za kupeleka waandishi ili taarifa zilizoendelea katika ziara ile na sisi kuzipata moja kwa moja. Sasa swali je utaratibu huu utaendelea au watakapokwenda China tu au viongozi wetu watakapokwenda nchi nyengine utaratibu huu utaendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo): Mhe. Spika, mpango huu utakuwa endelevu kadiri ya fedha zitakavyopatikana. Tulianza na viongozi wakuu Ambapo Mawaziri, Manaibu mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wawakilishi baadhi walipata fursa hiyo na watendaji. Sasa awamu moja ile tumemaliza lakini sasa unaendelea. Kwa kweli unakuja si moja kwa moja kwa kupitia Wizara ya Fedha peke yake hata nafasi nyengine zinakuja kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara nyengine. Kwa hivyo mpango huu wa kuelimisha watu wetu ni endelevu kwa lengo la kuwapatia fursa waweze kuona wenzetu walioendelea kama China wanafanya vipi na tujifunze kivitendo.

Nam. 51

Vitanda vya Uti wa Mgongo Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Hospitali za Serikali kwa muda mrefu zinakabiliwa na tatizo la ukosefu wa vitanda kwa ajili ya kuwapatia matibabu wagonjwa waliovunjika uti wa mgongo na kulazimika kulazwa katika vitanda vya kawaida kinyume na kanuni za matibabu kwa wagonjwa wa aina hiyo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupata vitanda hivyo.

(a) Kwa kuwa Pemba ndiyo kesi nyingi zinatokea kwa wachuma karafuu kuanguka na kuathirika uti wa mgongo; Je, Serikali ina mpango gani wa kupata vitanda kabla ya kumalizika kwa msimu wa uvunaji wa zao hilo la Karafuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake nam. 51 kama hivi ifuatavyo:-

Utaratibu wa upatikanaji wa vifaa vya hospitali katika Wizara uko kwa njia mbili. Aidha serikali inanunua au tunapata misaada kupitia wadhamini wa nje na wa ndani.

a) Mhe. Waziri wa Afya, Mkurugenzi Mkuu na daktari wa Mifupa wamekwenda India kwa ajili ya matayarisho ya wodi ya dharura *"Emergency Department*", na wamerudi tarehe 28 Septemba 2012 kutoka India kwa lengo la kuimarisha hospitali zetu na kutafuta misaada vikiwemo vitanda hivyo.

b) Tayari Serikali kupitia Wizara ya Afya imetiliana saini mkataba na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kuijenga upya Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani, ikiwemo kuipatia vifaa mbali mbali vya kisasa pamoja na vitanda maalum kwa ajili ya wagonjwa hao kwa kutilia maanani watakaopata ajali na watakaoanguka mikarafuu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri anayoendelea kuyatoa kwa kweli yanatia moyo na ya kuridhisha sana, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa hilo na vile vile nimpongeze tena kwa ujenzi anaoufanya kwenye hospitali ya Mnazi mmoja hivi leo asubuhi wa kuvunja sakafu, lakini nataka kumkumbusha vile vile katika kitengo cha ICU kuna mashimo mawili makubwa nayo asije akayasahau ali-*note* hilo.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa kuwa hospitali ni ujenzi wa muda mrefu haoni serikali ina mpango gani wa dharura ili wananchi wa kisiwa cha Pemba wanaovunjika katika mikarafuu kufanya utafiti huo.

Pili ujenzi wa hospitali hiyo utachukua muda gani na isije ikawa kama Uwanja wa Ndege wa kimataifa wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, vitanda kwa kweli nafikiri vitanda chochote sio lazima kile kinachopandishwa na kushushwa na *remote*. Utaratibu wa kukitayarisha kitanda kwa wagonjwa kama hao unaweza ukafanyika popote. Ni kitanda kile kile isipokuwa kinafanyiwa utaratibu wa kuekewa mbao. Kwa sababu kinachotakiwa pale ni kuhakikisha kwamba vitanda havibonyei. Kwa hivyo, hivyo ndivyo vinavyofanywa vitanda vilivyopo hapa na vilivyoko Pemba.

Kwa hivyo si leo tumeanza hiyo shughuli na wagonjwa wanatibiwa na wanapona. Lakini ukiwa na vitanda maalum inakuwa ni vizuri. Vinapopatikana vinakuwepo, sasa hivi tumehakikishiwa kwamba vitapatikana na Wachina katika vitu walivyotwambia kwamba tuombe tunachokitaka ili kuvitia katika hospitali ya Mkoani, kwa hivyo tulikuwa na *list* ya vitu ambavyo tunavijua kwamba tunavihitaji na vikiwemo hivyo vitanda.

Hospitali mkataba umetiwa mwezi uliopita na itachukua kama miezi minane kwa wao kukamilisha taratibu zote za huko kwao kupitia kutayarisha tenda, na wamesema kwamba watakapoanza watachukua mwaka mmoja na nusu kumalizika kujengwa.

Nam. 65

Uvunjaji wa Nyumba kwa Utengenezaji Barabara

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano katika kipindi cha kutengeneza barabara kuna watu nyumba zao ziliathirika kutokana na matengenezo hayo ya barabara.

(a) Ni watu wangapi nyumba zao ziliathirika.

(b) Wizara inayo orodha ya majina ya wale wote walioathirika, na ni kwa namna gani orodha hiyo imewekwa kwa uwazi ili wananchi hao waweze kuiona kwa urahisi.

(c) Je, kuna watu waliovunjiwa nyumba zao ambao bado hawajalipwa. Na ikiwa bado kwa nini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali namba 65 lenye vifungu (a) ,(b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo;

Wizara ya Miundombinu imetekeleza na inatekeleza miradi mingi ikiwemo miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara kwa Unguja na Pemba. Katika utaratibu tuliojiwekea katika miradi yote tunayoitekeleza hivi sasa sera ya serikali ni kuhakikisha kwamba hakuna mwananchi yoyote atakayevunjiwa nyumba yake kwa ajili ya ujenzi wa barabara kabla ya kulipwa fidia inayostahiki.

Mhe. Spika, malalamiko mengi yahusuyo majengo huwa yanatokea wakati wa utekelezaji wa mradi husika au baada ya mradi wenyewe. Na sababu kubwa ni kwamba, maumbile ya nyumba zenyewe, maumbile ya ardhi husika pamoja na ukaribu wa nyumba husika na barabara inayojengwa. Aidha napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba tutaendelea na sera hii ya kutovunja nyumba ya mwananchi yoyote kabla ya kumlipa fidia. Lakini pia kwa upande wa vipando na mazao naomba wananchi watuvumilie na azma ya serikali ni kuona kwamba hali ya fedha ikiruhusu madeni hayo yatalipwa au kupatiwa ufumbuzi.

Hata hivyo malalamiko yote yatokanayo na kubomoka kwa nyumba baada ya ujenzi yamekuwa yakiongezeka kwa kasi ajabu sana. Kwa mfano katika miradi miwili mikubwa ya barabara za Amani/Dunga na Mfenesini/Bumbwini zaidi ya watu 30 wamejitokeza na malalamiko hayo.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Kwa upande wa Barabara tuliyoitaja ya Mfenesini – Bumbwini na Amani – Dunga jumla ya wananchi 34 wamejitokeza kudai fidia zao baada ya ujenzi wa barabara hizo kukamilika.

(b) Wizara inayo orodha ya majina ya wale wote walioathirika na ujenzi wa barabara kama nilivyotangulia kueleza hapo juu, Wizara itatekeleza miradi mingi, orodha ya majina ya nyumba zilizoathirika katika mradi wa barabara kuu Zanzibar utaambatanishwa na utapatikana. Msingi ni kwamba wanaodai wote orodha yao ipo na iko wazi.

(c) Hakuna mwananchi yeyote aliyevunjiwa nyumba yake na hajalipwa fidia yake, na hajalipwa fidia kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya barabara.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali dogo moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi kwamba iko haja kupata orodha za watu wote ambao nyumba zao zimevunjwa na zilizoathirika ili kujua kama fidia zao zimelipwa kwa kila mtu ambaye amehusika, yaani sisi tuweze kupata orodha kwa sababu watu wanatufuata sisi kujua kwamba mimi sijalipwa. Kwa hivyo ili kuondosha hili tatizo katika eneno langu ningependa tuwe na orodha za majina ya watu wote ili tuweze kufuatilia aliyelipwa na asiyelipwa. Je, inawezekana kupatikana orodha hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, msingi mkubwa ni kuhakikisha kwamba kila anayestahiki mwenye haki kulipwa fidia. Na sisi katika utaratibu wetu tumejiridhisha kwamba hakuna mwananchi ambaye tumemvunjia nyumba pasi na kumlipa fidia. Lakini wazo la Mhe. Mwakilishi mimi nalikubali kwamba kuna haja ya kuwa na hiyo orodha ambayo itafafanua zaidi. Kwa maana yule ambaye amevunjiwa nyumba na kulipwa fidia na wale ambao nyumba zao zimeathirika aidha wawe wamelipwa au hawajalipwa taarifa hizo tutampatia na tunakuomba uendelee kutupa ushirikiano katika kufanikisha jambo hilo.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Mhe. Naibu Waziri wakati wizara yako inapofanya mpango wa *survey* wa kutaka kujenga barabara baadhi ya nyumba zao hazimo katika mpango ule wa kuvunjwa. Lakini wakati zoezi la ujenzi linapoendelea, baadhi ya nyumba huvamiwa na maji ya mvua na nyumba zile zikaweza kuanguka. Je, wizara yako ina mpango gani wa zile nyumba ambazo hazikuwemo katika mpango wa ujenzi lakini katika ujenzi unapoendelea zikaanguka kwa mvua, wizara yako ina mpango gani wa tathmini wa watu hawa ambao nyumba zao zimefikwa na athari hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, sababu kubwa ya serikali kulipa fidia kwa ajili ya nyumba ni kupisha vizuizi ili kutekeleza mradi husika wa barabara. Sasa jambo la kujikumbusha ni kwamba kuna sheria inayosimamia barabara na wajibu wa wananchi ni kujenga katika maeneo ambayo yameruhusiwa kwa mujibu wa taratibu na sheria husika. Sasa tunalipa fidia kwa zile nyumba ambazo zitakuwa kikwazo cha kutekeleza mradi husika wa barabara. Na tumeeleza kwamba nyumba ambazo zitakuwa zinaathirika wakati wa utekelezaji wa mradi wa barabara huwa tunaziorodhesha na hicho kinakuwa kipaumbele namba mbili katika ulipwaji wa fidia.

Ulipwaji wa fidia wa kwanza ni kuhakikisha ile nyumba husika inayozuia upitishaji wa ile barabara ndio tunayoipa kipaumbele. Sasa Mhe. Mwakilishi kama kutakuwa kuna nyumba ambayo inaingia maji kwa sababu ya ujenzi wa barabara jambo hili hatutokuwa tuna majibu ya moja kwa moja. Ni suala ambalo linahitaji tukae tuangalie hayo mazingira halisi yapo vipi baadae tutaona namna gani tunaweza kuwasaidia wananchi hao.

Tunasema hayo kwa kuwa na uzoefu, kuna watu ambao wamekwenda kujenga katika maeneo yanayopita maji na ujenzi wa barabara tunalazimika tuinyanyue ili kuikinga barabara yetu iweze kudumu kwa muda mrefu. Sasa kama mtu kajenga katika eneo la maji, kisingizio chako kwamba barabara imenyanyuliwa kwa hivyo tutakuwa hatuna sababu ya kumlipa fidia. Lakini kama kuna maeneo ambayo sisi tumesababisha maji yaende kwake kwa hivyo tuna haki na tuna sababu ya kukaa ili kuona kwa kiasi gani tunaweza kumsaidia, kwa sababu itakuwa tumemsababishia athari katika nyumba yake.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, katika utengenezaji wa barabara inayotoka Konde kuja Wete katika eneo la Kinyasini, wakati barabara ilipotengenezwa kuna nyumba za wakaazi zisizopungua kumi ziliharibika na wengine wakahama katika majumba yao, na katika kulifuatilia Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano alitaka kupata ushahidi na nikamletea barua ya Sheha na saini yake na mhuri wa wale watu wameharibiwa kweli na walivyoahidi kuwa watawalipa lakini hawajawalipa mpaka leo. Na wale watu wanahangaika na maisha je, haoni kuwa Mhe. Waziri kufanya hivi kutowafanyia haki wananchi hawa sasa hivi hawana pa kukaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kama kuna ahadi ya Mhe. Waziri serikali itaitekeleza, lakini kuchelewa kwetu huko haimaanishi kwamba hatuwatendei haki wananchi hao. Tumeeleza hapa kwamba utaratibu wetu ama sera ya serikali ni kuhakikisha wale ambao nyumba zao tunavunja kwa ajili ya kupisha mradi wa barabara hatutovunja kabla ya kumlipa fidia. Lakini kama kuna nyumba ambazo zitaathirika wakati wa utekelezaji au baada ya utekelezaji hilo litakuwa kipaumbele namba mbili katika ulipaji wa fidia. Tunasema hivyo kwa kutambua kwamba tuna maeneo mengi ambayo tunatekeleza miradi, tuna tatizo la upatikanaji wa fedha, na tuna mambo ambayo tunalazimika kuwalipa fidia watu ili kunusuru miradi yetu.

Kwa hivyo nimuombe tu Mhe. Mwakilishi, endelea kuwa na imani na sisi, endelea kushirikiana nasi, tutapokuwa na fedha ya kukidhi tutakwenda kuwalipa fidia wananchi hao kwa sababu tunaamini kama wameathirika wana haki ya kulipwa fidia kwa mujibu wa taratibu na sheria husika.

Nam. 7

Shirika la Umeme

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Shirika la Umeme ni Shirika la Serikali, kwa hivyo huendesha shughuli zake kupitia fedha za walipa kodi wa nchi hii bila kujali itikadi zao za vyama au wapi wanatoka. Kwa upande wa Pemba kuna malalamiko kwamba katika Shirika hili ajira zinatolewa kwa misingi ya ubaguzi sambamba na kutofuatwa kwa sheria za utumishi ikiwa ni pamoja na kuwaajiri vijana bila ya Mikataba na hatimae kusitisha ajira zao kinyume na taratibu.

a) Je, malalamiko haya ni ya kweli.
b) Kama ni kweli ni sababu zipi za msingi zilizopelekea kufanyika hivyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibuu Mheshimiwa suali lake namba 7 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kadri wizara yangu inavyoelewa ajira ndani ya shirika hufanywa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu ziliopo. Lakini Mhe. Spika, kwa kuwa jambo hili ni miongoni mwa hadidu rejea za Kamati maalum iliyoundwa kufuatilia malalamiko kadhaa likiwemo hili la ajira dhidi ya Shirika la Umeme, ni vyema mjadala wa hoja hii ukasubiri ripoti ya Kamati hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri kasema kwamba swali langu ni sehemu ya hadidu rejea za Kamati Teule, ingawa Kamati Teule si mahkama kwamba neno likiwepo mahkamani halihojiwi, basi kwa heshima na taadhima nadhani nisiulize swali la nyongeza nikubaliane na hoja yake. Ahsante sana.

Nam. 58

Kuanzisha Vitengo vya Utafiti

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Serikali ya awamu ya saba imeamua kuanzisha viatengo vya Utafiti na Mipango katika kila Wizara ili sera na sheria zitokane na utafiti kabla ya kutungwa na serikali.

a) Je, ni tafiti ngapi tayari zimefanyika hasa katika mazao ya Kilimo na Biashara Zanzibar.
b) Serikali itaweza vipi kumudu gharama za utafiti hasa katika mambo ya kilimo wakati vyuo vyake vingi vinakabiliwa na ufinyu wa bajeti za utafiti.
c) Kwa kuwa Chuo cha Kilimo Kizimbani ni tegemeo kubwa katika sekta ya Kilimo, Serikali imechukua hatua gani kukiimarisha Chuo hicho ili kisaidie mambo ya utafiti nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele yako katika Baraza lako tukufu. Pili napenda kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunivumilia na kunipa ruhusa ya kujibu swali la Mheshimiwa ambalo ndio kwanza leo nisimame katika Baraza hili tukufu.

Pia niruhusu niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi *back bencher* ambao tangu juzi walikuwa wananionea huzuni na huruma sana kwa kutwikwa mzigo huu mzito, lakini Mhe. Spika, napenda kusema kwamba huruma hizo na huzuni hizo zisiwe huruma za mamba, wanisaidie, naomba msaada wao.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 58 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali lake lenye vipengele (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Tangu mwezi wa Novemba 2010 ilipoingia madarakani Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya awamu ya saba sasa imeshatimiza karibu miaka miwili ya uongozi. Ndani ya kipindi hiki serikali imeanzisha utafiti wa kilimo Zanzibar wa sheria namba 8 ya mwaka 2012.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki tafiti mbali mbali zimefanyika na nyengine bado zinaendelea zikiwemo za mazao ya chakula pamoja na tafiti zinazohusiana na udhibiti wa maradhi ya mimea hasa katika mazao ya mpunga na muhogo. Tafiti za kutathmini aina tofauti za mbegu za mazao ya Chakula na mboga mboga na ambazo zinastahmili maradhi ya hali ya hewa ya Zanzibar.

Tatu, tafiti zinazohusiana na ukusanyaji, utunzaji na uhifadhi wa mbegu tofauti za kienyeji zikiwemo za mazao ya chakula na biashara kama mpunga, muhogo, migomba na mazao ya viungo pamoja na uzalishaji na usambazaji wa mbegu mama kwa mazao ya chakula. Kujenga na kukarabati miundombinu ya utafiti ikiwemo maabara za mazao.

(b) Mhe. Spika, baada ya Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzíbar kuanzishwa, Uongozi wa Taasisi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili imeanza mchakato wa kutekeleza sheria hiyo kwa vitendo. Sehemu ya 16 ya Sheria ya Taasisi inazungumzia jinsi ya taasisi itakavyopata fedha kwa ajili ya kuendesha kazi zake ambazo ni pamoja na:

i. Fedha zitakazotolewa na serikali kwa njia ya ruzuku (*subvention*) kama zitakavyokubaliwa na Baraza la Wawakilishi kwa kazi za taasisi;
ii. Fedha zitakazolipwa taasisi kutokana na kazi zake;
iii. Misaada, michango, zawadi kutoka taasisi nyengine au watu binafsi na fedha nyengine zitakazolipwa taasisi kwa njia ya *fees*, michango kutokana na kazi itakazofanya.

(c) Mhe. Spika, rasilmali watu ni nyenzo muhimu katika kazi za utafiti. Rasilmali hii inahitaji kuandaliwa ili kufanya kazi za utafiti. Chuo cha Kilimo Kizimbani kimechukua hatua ya kuwa andaa walimu wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi, lengo likiwa ni kuwajengea uwezo ili waweze kutoa mafunzo kwa ufanisi pamoja kufanya kazi za utafiti kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Zanzíbar.

Mhe. Spika, hivi sasa chuo kina walimu 11 ambao wana uwezo wa kushiriki katika kazi za utafiti. Walimu hao wanavyo viwango vya elimu ngazi ya digirii ya pili wanne (4) na digirii ya kwanza saba (7). Aidha, kati ya mwaka 2011 na 2012 chuo kimepeleka jumla walimu 10 katika mafunzo ya ngazi ya digirii ya pili katika fani tofauti. Walimu watano kati yao wako katika hatua za kufanya utafiti kwenye maeneo ya uzalishaji mazao, mifugo na utunzaji. Tuna imani kwamba walimu hawa watakua na uwezo mkubwa wa kuchangia kwa asilimia kubwa katika kufanikisha kazi za utafiti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri mpya naomba niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa mabadiliko ya tabia ya nchi yameathiri sana hali ya hewa ya Zanzíbar ikiwemo ukosefu wa mvua. Je, ni kwa kiasi gani mazao ya biashara kama vile karafuu uzalishaji wake umeathirika katika kipindi hichi. Hilo la kwanza.

Pili, serikali ina mpango gani endelevu wa kuweza kuanzisha mazao yanayostahamili ukame kutokana na tabia ya nchi kuwa mvua ni ndogo badala yake kuachana na hayo yanayohitaji mvua kubwa sana kama vile karafuu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kesi yake ni ngumu kwa kijana wetu, lakini nitamjibu mimi *In sha Allah*.

Mhe. Spika, ni kwamba tabia ya nchi imebadilika na ni kweli baadhi ya mazao yameathirika, lakini tukitembea tutizame kwamba katika hali hii ya jua huwa ndio inazaa sana na ikija mvua huwa uzazi unapungua. Tutizame miembe, miembe sasa hivi inazaa mara tatu, hivi sasa ukipita kwenye muembe una maua ya aina tatu, kuna embe pevu, kuna embe za kati na kati na kuna maua. Sasa kuathirika kwa mazao kama aliyoyazungumza yeye kama karafuu basi karafuu nazo wakati wa jua huzaa sana tofauti na wakati wa mvua kuwa zinachanua majani. Hii *research* wanaendelea na chuo cha kilimo pale Kizimbani na baada ya muda nafikiri watatoa taarifa yao ya namna wanavyoendelea katika hili.

Halafu suala lake la pili mkakati wa kuwaelimisha watu kulima mazao yanayohimili ukame. Hilo vile vile Wizara ya Kilimo wanahimiza sana kulima mazao ambayo yanaweza kuhimili ukame isipokuwa yanakuwa na matatizo kidogo. Kwa mfano, muhogo unahimili ukame ila muhogo ukipata jua unakuwa mchungu, mbaazi zinahimili ukame lakini hili suala alilosema kutoa taaluma na mkakati Wizara ya Kilimo itajitahidi kuwafundisha wananchi kulima mazao yanayohimili ukame katika kipindi hiki ili kuondoa athari zinazosababishwa na matatizo haya ahsante sana.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru nami kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza dogo tu. Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzíbar hivi sasa inaathirika sana kwa mazao yake takriban mazao yote yana magonjwa tofauti, na Chuo chetu cha utafiti ni chuo kimoja cha kilimo ambacho kiko Kizimbani hapa Zanzíbar. Je, kwa kuwa magonjwa haya ni mengi na chuo ni kimoja tu serikali ina mpango gani wa kuongeza Chuo chengine cha kilimo ili kusaidiana na Chuo cha Kizimbani katika kufanya utafiti na kufundisha watu kilimo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, hivi sasa tuna jitihada kubwa ya kukikuza Chuo cha Kilimo kwanza cha Kizimbani kifikie hatua ya uwezo mkubwa zaidi wa kufanya tafiti, ndio maana hata katika jibu la msingi Mhe. Naibu Waziri ameeleza kwamba wanakuzwa wale walimu wanaosomesha katika Chuo cha Kizimbani ili waweze kufikia kiwango cha kufanya utafiti, wakishafikia hatua ya kukua wale na kuwa tayari sasa hivi wanaweza kushiriki katika tafiti basi nafikiri rai yake ya kuanzisha na chuo chengine Pemba ni rai nzuri sana na tutaitekeleza *In sha Allah*.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa kuteuliwa na bila shaka *backbencher* watakuwa na huruma lakini wasisahau kwamba huruma hailei mwana. Mhe. Spika, baada ya nasaha hizo naomba niulize swali la nyongeza. Hivi sasa dunia inakabiliwa na suala zima la utapia mlo na Tanzania ni miongoni mwa nchi kumi ambazo zinaongoza kwa tatizo la utapia mlo hasa kwa watoto wadogo. Wataalamu wa afya duniani wanasema kwamba viazi vitamu rangi ya njano vinapendekezwa sana kwamba vitumike katika maisha ya chakula cha watoto. Hebu naomba waziri anambie wizara yake imefanya utafiti gani

kujua viazi hivi vina faida gani ya ziada na je, vitamini gani vinapatikana katika viazi hivi ili tuweze kutumia katika maisha ya watoto wetu ili kuondosha utapia mlo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, ni kweli kama anavyosema viazi vile vya rangi ya njano (viazi mzungu) Mheshimiwa anasema hapa ni vizuri sana kwa lishe, hata wagonjwa wa UKIMWI wanashauriwa sana kutumia viazi vile vya rangi ya njano.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, anazungumzia tumefanya utafiti gani. Siwezi kumjibu hapa itabidi niwasiliane na chuo kwamba katika suala hili wamefanya utafiti kiasi gani na hiyo nitamjibu kwa maandishi ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri tunawashukuru sana, ingekuwa niko kwenye mkutano wa siasa ningesema tumuongeze makofi.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi hii niulizie kuhusu utaratibu, natumia kanuni ya 42 ya kujadili jambo la dharura linapotokea. Mhe. Spika, Jana majira ya saa saba mchana hadi wakati huu katika Mji wa Zanzíbar kulitokea vurugu kubwa zilizopelekea uvunjifu wa amani, uharibifu wa mali, hofu kwa jamii hata kusitisha shughuli za kijamii na za kiuchumi.

Mhe. Spika, kwa kuwa tukio hili lilitokea kufuatia kutoweka katika mazingira ya utatanishi kwa mwananchi mwenzetu na kwa kuwa ni jukumu la msingi la serikali chini ya ibara ya nane na ya tisa ya Katiba ya nchi yetu linaloipa mamlaka kulinda amani na utulivu sambamba na kulinda amani na usalama wa nchi na raia wake. Mhe. Spika, kwa uzito wa suala hili naomba Baraza lako tukufu liakhirishe kwa muda shughuli zake zilizojipangia kwa wakati huu ili sisi Wawakilishi wa wananchi tuweze kujipa nafasi ya kushauriana na serikali katika kukomesha vitendo hivi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa sababu jambo hili ni zito limegusa nchi yetu, limegusa serikali na jamii naomba tutumie kanuni hii ili jambo hili tulijadili kwa muda uliowekwa katika kanuni yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Hii hoja inaonekana imeungwa mkono lakini mimi ningependa tukajua tunalifanyaje, kwa sababu tunaweza kuakhirisha lakini tukasambaa bila ya kazi yoyote ya kufanya juu ya hili wakati huku muda uliobaki kufanya shughuli zetu za mkutano huu bado hatujazimaliza. Nafikiri mtakumbuka kwamba tumebaki kwa siku kama tatu jioni hatupiti kwa sababu ya shughuli zetu kuwa hazijaandaliwa vizuri, mpaka jana ilionekana kwamba hatutaweza kuendelea na mswada. Suala ni muhimu lakini tunafanya nini? Hoja inaweza ikapita lakini tukatoka hapo nje tukasambaa kila mmoja akenda nyumbani kwake ikawa hatukufanya kitu, muda umepotea na kwa kweli itakuwa si jambo la busara. Tusikilize serikali wanasema nini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi na pia nimshukuru ndugu yangu Mhe. Omar Ali Shehe kwa kueleza jambo ambalo kwa kweli serikali na wananchi limewagusa sana. Ni kweli jana kumetokea vurugu na serikali ilitoa taarifa, na kwa sababu Mhe. Mjumbe ameelezea masikitiko yake kuhusu jambo hili na ni kweli wananchi wetu wengi wamefanya hofu kutokana na hali iliyojitokeza, lakini hivi sasa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinakutana kuifanyia tathmini hali hii na taarifa yao baada ya muda usio mrefu itapatikana. Kwa hivyo, ningeomba Baraza lako hili na Mhe. Mwakilishi waendelee kuvuta subira na serikali itakuwa inatoa taarifa kadiri ya hali inavyoendelea. Lakini nataka nipende kulihakikishia Baraza hili kwamba vyombo vyote vya ulinzi na usalama vimedhibiti hali hiyo na hali sasa ni tulivu na hatua kali zitachukuliwa kwa wale wote waliohusika kufanya vurugu hizo.

Vile vile Jeshi la Polisi linaendelea kufanya uchunguzi na kumtafuta Sheikh Farid Hadi Ahmed kujua nini chanzo cha tatizo na kwa nini limetokea lililotokea. Kwa hivyo, nalo hilo linafanyiwa kazi, ningependa wananchi wetu na Baraza hili tukufu tuendelee kuvuta subira.

Jambo la msingi hapa Mhe. Spika, ni kwa wananchi kufuata taratibu za sheria, kukiuka utaratibu wa sheria kunaweza kuitia nchi katika matatizo magumu sana na tukawa sote katika hali ngumu sana hasa vitendo vya uchochezi vinavyofanywa na kikundi kimoja kufanyia kikundi chengine ama kwa njia moja au nyengine kwa wananchi kufanya uchochezi kwa mwananchi mwengine hasa kama yale yanayohusiana na vyama hata suala

lililotokea la kuchoma moto maskani za CCM jambo hili linaweza kuzaa mtafaruku mkubwa kwa sababu na wananchi hao wana CCM wanaweza kuamua na wao kulipa kisasi jambo ambalo litaleta vurugu kubwa katika nchi yetu.

Kwa hivyo, naomba sana wananchi wote tuwe watulivu wakati huu serikali inalifanyia kazi jambo hili na nataka nilihakikishie Baraza hili tukufu kwamba wale wote waliohusika hatua kali za kisheria zitachukuliwa na nchi itaendelea kuwa katika hali ya amani na utulivu. Naomba tuvute subira Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mimi nafikiri tuendelee na shughuli zetu kwa sababu jambo lenyewe liko tete na kanuni hii aliyosema Mhe. Mjumbe inataka tujadili ndivyo inavyosema, tuakhirishe shughuli zetu ili tujadili hili jambo lenyewe liko kwenye utafiti na taarifa ya serikali jana usiku ilitoka. Sasa tukijadili tunajadili juu ya jambo ambalo utafiti wake unaendelea, nina wasi wasi muda utakwenda tunaweza tukazungumza lakini ikawa ni kutaka serikali itoe maelezo, nadhani ndicho kitakachokuja itoe maelezo juu ya jambo ambalo utafiti wake unaendelea.

Sasa mimi naamini kwa taarifa ya jana ya hali ya mambo iliyotoka na muendelezo wa jambo hilo kulifuatilia naamini serikali itatoa taarifa nyengine baadae juu ya jambo hili. Hivi sasa tusivunje mtiririko wa shughuli zetu tuendelee nazo kwa sababu kwa kadiri ninavyoliona jambo lenyewe lilivyo tunafuatiliaje juu ya mtu ambaye haeleweki alipo, mana tofauti na masuala mengine ambayo tuliwahi kuamua meli ilipozama ili tushirikiane na wananchi katika suala lile mfano, lile lilikuwa linaeleweka kwamba kuna jambo kubwa ndani ya nchi na hili si dogo lakini namna ya ufuatiliaji wake kuufanya humu ndani tulimo kidogo nadhani itakuwa inaleta matatizo, niamue basi tuendelee na shughuli zetu na serikali iendelee kufanya utafiti juu ya hilo.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira ya Mwaka 2012

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kunivumilia hapo jana ili leo nipate nafasi kuwasilisha mswada huu baada ya kutoka safari. Naomba radhi vile vile sauti yangu imeingiliwa na wageni kidogo.

Mhe. Spika, tarehe 11 na 12 mwezi huu tulipitisha Mswada muhimu sana hapa unaohusu Afya ya Jamii. Mswada ule utaweza tu kufanya kazi vyema kama watakuwa watekelezaji wana uwezo na nguvu za kisheria na kama unakumbuka wakati wa mjadala hapa yalizuka masuala mengi sana kwamba hizi kazi zitafanyikaje, sheria hii ngumu, kumbe ilikuwa mswada huu bado wakati wake haujafika ili kuja kusaidia jinsi ya kuutekeleza mswada ule. Kwa hivyo, mswada huu unaohusu maofisa wa afya ambao ndio watakaokuwa wasimamizi wa shughuli za afya na mazingira unakusudia kuweka utaratibu bora wa kuwatambua, kuwasajili na kuwapa leseni maafisa wa afya, jamii na mazingira ambao kwa mufa mrefu wamekuwa wanafanya kazi zao bila ya kuwepo kwa utaratibu wa kisheria na kuwatambua.

Mhe. Spika, mswada huu una vifungu 39.

Sehemu ya Kwanza
Utangulizi

Jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika sheria iliyopendekezwa pamoja na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika katika mswada huu.

Sehemu ya Pili
Kuanzishwa kwa Baraza

Sehemu hii ina vifungu 12 kuanzia kifungu cha 3 hadi kifungu cha 14.

Kifungu 3 Kuanzishwa Baraza litalojulikana kama Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira.
Kifungu 4 Kinahusu muundo wa Baraza
Kifungu 5 Kazi za Baraza

Kifungu 6 Uwezo wa Baraza
Kifungu 7 Taasisi inakusudia kutoa mafunzo ya afya ya jamii
Kifungu 8-14 Vimejumuisha vikao vya Baraza, akida, mkutano, uwakilishi, maoni ya Baraza, amri na maelekezo mengine ya Baraza, malipo kwa Wajumbe na kumbukumbu za vikao.

Sehemu ya Tatu
Usajili na Utoaji Leseni

Sehemu hii ina jumla ya vifungu vinane,
Kifungu 15 Mrajis wa Baraza
Kifungu 16 Kazi za Mrajis
Kifungu 17 Usajili na Utoaji Leseni
Kifungu 18-19, 20, 21 na 22 vinahusu malipo ya usajili na leseni kuomba tena leseni, usajili wa wageni, usajili wa muda na uwezo wa kusitisha kufuta na kuondoa usajili.

Sehemu ya Nne
Masharti ya Adhabu

Sehemu hii ina jumla ya vifungu nane

Vifungu vya 28-30 Mrajis kupokea malalamiko, uchunguzi wa Baraza, taratibu ya uchunguzi, uwezo wa Baraza wa kutoa adhabu, uwezo wa kuita shahidi, kinga kwa shahidi, rufaa zidi ya uamuzi wa Baraza na kuwasilisha shauri Mahkamani.

Sehemu ya Tano
Makosa na Adhabu

Sehemu hii ina jumla ya vifungu vitano vifungu vya 31 hadi 35 vinavyohusu adhabu kwa kufanya kazi bila ya ruhusa, makosa kwa kujipatia usajili na leseni kinyume a utaratibu, adhabu kwa wasiheshimu maagizao ya Baraza, adhabu ya jumla na adhabu bila ya mashtaka.

Sehemu ya Sita
Masharti ya Fedha

Sehemu hii ina jumla ya vifungu vine navyo ni 36 – 39 na vinahusu chanzo cha fedha kwa ajili ya Baraza, matumizi, ukaguzi, na uwezo wa waziri kuunga kanuni.

Mhe. Spika, naomba Wajumbe waujadili, watoe maoni na nawashukuru sana Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii wameupitia na kufanya masahihisho yenye kustahiki.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Tumkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Hakuna Mjumbe aliyeachiwa kazi hiyo na Mwenyekiti?

TAARIFA

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, mimi ni Makamo Mwenyekiti wa kamati hii, lakini hadi nafika hapa sina taarifa ya kuachiwa kazi hii na kwa hivyo kwa kadiri ya uwezo wangu siwezi kuisoma. Kwa sababu nimekwenda ofisini kwa Katibu nimeuliza nimeambiwa kwamba Mwenyekiti atakwenda mwenyewe kusoma na sijapewa taarifa ndio napewa hapa mbele yako. Kwa hivyo sina uwezo wa kuisoma haraka haraka hiyo.

Mhe. Spika: Je, kuna Mjumbe mwengine, Mjumbe ambaye atasoma kwa niaba ya kamati?

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutujaalia uzima, afya na uwezo wa kutoka katika maeneo yetu mpaka kufika katika jengo hili bila ya kushikiliwa. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote hatuna budi kumshukuru.

Ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Spika, nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kukushukuru wewe uliyenipa fursa hii ili kuja kutoa maoni ya kamati japo kwamba hii karatasi ndio kwanza naipata humu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe nitawaomba radhi kwa mapungufu yote yatakayojitokeza wakati nawasilisha taarifa hii kwa sababu mimi ndio kwanza nimeiona humu, sikupata muda wa kujitayarisha. Kwa hivyo, kwa niaba ya Mwenyekiti wa kamati yetu naomba kuwasilisha taarifa hii.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima wa afya ili kuwasilisha mchango wa kamati yetu kuhusu Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya na Jamii na Mazingira na kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira.

Mhe. Spika, aidha shukurani zangu ziwafikie Wajumbe wa Kamati na Watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa mashirikiano ya kutosha wakati wa kuupitisha na kuuchangia mswada huu. Napenda kusema kwa niaba ya kamati tunawashukuru kwa dhati watendaji hao.

Mhe. Spika, ningependa pia nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Wizara na Wanasheria wetu wa Baraza kwa kutoa mchango wao, kwa kutupa muongozo na ufafanuzi wa baadhi ya mambo wakati wa kuupitia na kuuchangia mswada huu.

Mhe. Spika, ni vyema kuwataja Wajumbe wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ambao walihusika katika kuupitia mswada huo. Wajumbe hao ni:-

1. Mhe. Amina Iddi Mbarouk	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Hija Hassan Hija	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdu	-	Mjumbe
4. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Mjumbe
5. Mhe. Ashura Sharif Ali	-	Mjumbe
6. Mhe. Nassor Salum Ali	-	Mjumbe
7. Mhe. Saleh Nassor Juma	-	Mjumbe
8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Mjumbe
9. Ndg. Asha Said Mohamed	-	Katibu
10. Ndg. Talib Enzi Talib	-	Katibu

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa niende moja kwa moja katika mswada husika.

Mhe. Spika, mswada huu wa sheria umelenga kuweka utaratibu mzuri wa kuwatambua, kuwasajili na kuwapa leseni maafisa wa afya ya jamii na mazingira ambao kama tulivyoeelezwa kwa muda mrefu wamekuwa wakitoa huduma kwa jamii bila ya kutambuliwa.

Hali hii Mhe. Spika, ingeweza kupelekea kuwa na mrundikano wa maafisa wa afya ya jamii ambao hawana sifa za kutoa huduma hizo na hatimaye jamii kuathirika. Kwa hatua hiyo tunaipongeza wizara na Serikali kwa ujumla kuona umuhimu wa kuwepo kwa sheria maalum itakayowatambua maafisa hao ili waweze kutoa huduma kwa mujibu wa sifa walizonazo na zinazotambulika kisheria.

Mhe. Spika, mswada uliopo mbele yetu unawatambua wasaidizi maafisa wa afya ya jamii kuwa ni wale wenye sifa ya ngazi ya Diploma. Hata hivyo wapo wasaidizi maafisa wa afya ya jamii ambao wana sifa ya vyeti wana uzoefu wa muda mrefu. Kamati imeona umuhimu wa kuendelea pia kuwatambua wafanyakazi hao kama wasaidizi wa

maafisa wa afya ya jamii. Mhe. Spika, imeonekana kuwa maafisa hao ni wengi na wanaweza kusaidia kwa njia moja au nyengine katika kutoa huduma hizo za afya za mazingira.

Mhe. Spika, sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira imelenga pia kuanzisha chombo maalum kitakachosimamia pamoja na mambo mengine, usajili wa utoaji wa leseni kwa maafisa wa afya na mazingira ambacho kitajulikana kama Baraza wa Afya na Mazingira.

Kamati yetu kwa upande wake Mhe. Spika, imeona kuwa chombo hiki kimepewa kazi nyingi ambapo utekelezaji wake unaweza kuwa ni ngumu. Hivyo kamati inashauri kuwepo kwa chombo chengine ambacho wizara itaona kinafaa ili kulipunguzia majukumu mengi Baraza hilo. Kwa mfano kifungu cha 5 (1) (c) na (g). Majukumu waliyopewa Baraza yapelekwe katika chombo chengine.

Mhe. Spika, kama sheria inavyoelezwa kuwa mtu yeyote anayetoa huduma kama Afisa wa afya ya jamii na mazingira bila ya kuwa na leseni au aliyesimamishwa kutoa huduma na kuendelea kutoa huduma atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani awajibishwe kwa adhabu kwa mujibu wa sheria. Hivyo kamati yetu inahimiza wizara kuhakikisha kuwa sheria ya Usajili ya Usamamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira itakayopitishwa inasimamiwa ipasavyo.

Mhe. Spika, kimsingi kamati imekubaliana na mapendekezo ya rasimu ya mswada. Hata hivyo imefanya baadhi ya marekebisho madogo madogo yakimaandishi pamoja na kurekebisha baadhi ya vifungu.

Kwa mfano kifungu cha 2 (Ufafanuzi). Katika tafsiri ya neno leseni kimeainishwa kifungu cha 16 ambacho kimefanyiwa marekebisho na kisomeke kifungu cha 17. Aidha katika tafsiri ya neno Mrajis, kumeainishwa kifungu cha 14 ambacho pia kimefanyiwa marekebisho na kisomeke kifungu cha 15.

Mhe. Spika, kamati yetu pia iliona haja ya kuzingatiwa tafsiri ya neno mgeni, kwa kuzingatia kuwa wapo waafisa wa afya wa jamii na mazingira ambao huingia nchini kwa ajili ya kutoa huduma hizo.

Mwisho Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana, naunga mkono hoja na naomba radhi kwa mapungufu yaliyojitokeza katika kuwasilisha hotuba hii kwa sababu matayarisho nilikuwa sina.

Naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutuwezesha asubuhi hii tukakutana hapa tukiwa ndani ya hali ya afya na uzima na ikiwa kuna wenzetu Mwenyezi Mungu kawajaalia hawakufika katika ukumbi huu kwa matatizo yao au matatizo mbali mbali, tunaomba Mwenyezi Mungu awape wepesi ili tuweze kushirikiana nao.

Mhe. Spika, mimi nimesimama hapa kwa kupitisha sheria hii ambayo kuwa ni Sheria ya Usajili ya Usimamizi wa Afya ya Jamii na Mazingira na kuanzishwa Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwa sababu mswada huu unajumuisha mswada uliopita kwa kupewa nguvu na uwezo maafisa hawa kufanya kazi yao kama madhumuni na sababu yanavyoeleza, kuwa mswada huu unavyokusudiwa kuweka utaratibu bora wa kuwatambua wasajili na kuwapa leseni maafisa wa afya ya jamii na mazingira ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakifanyakazi zao bila ya kuwepo kwa utaratibu wa kisheria na kutambuliwa.

Kwa hivyo mimi Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu pamoja na marekebisho yake yote na wananchi wangu wa Wilaya ya Micheweni asilimia 100 kwa 1000. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuchangia mswada ulio mbele yetu mswada wa sheria wa Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwanza kabisa Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima pamoja na wenzangu waliohudhuria katika Baraza lako tukufu Mwenyezi Mungu atujaalie na zaidi wapate afya njema.

Mhe. Spika, vile vile nikushukuru wewe kwa hekma zako na busara unazotuendesha katika Baraza hili, nilikuwa nasikia tu na mimi nilikuwa najifundisha humu lakini busara zako na hekma zinatuonesha wazi kama ni mzoefu wa kuliendesha Baraza hili.

Lakini pamoja na hayo napata masikitiko makubwa sana kuwa Baraza letu linatia aibu. Juzi tu tulikaa hapa ukatupa maelekezo lakini ukiliangalia Baraza leo linatisha, Wajumbe wengi humu hawamo na sababu hatujui.

Mhe. Spika, pili nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Afya pamoja na watendaji wake kutuletea mswada huu ambao nasema ni mzuri sana, kwa sababu ni binadamu na mazingira ndio afya.

Mhe. Spika, pia nisiwe mwizi wa fadhila, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi Mussa Aboud Jumbe, siku ya tarehe 13 kwa kwangu mimi nasema ni historia, alifanya doria ndani ya Zanzibar hii kwa anga na kwa bahati nzuri akamualika mtu wa Jumuiya ya Wavuvi ambao ni jamii ya Kikojani (KOFIDO). Hivi tunashukuru sana na Wakurugenzi wengine na maafisa waige mambo kama hayo kwamba jambo lolote unalolishirikisha jamii basi litapata muafaka zaidi kuliko kuwatenga, ninampongeza sana.

Mhe. Spika, mswada wetu huu ni maafisa kwa kuweka maafisa mazingira na ustawi wa jamii. Ni kweli jambo hili lolote kama halina usimamizi basi haliwi zuri lakini nasema wizara imeamua kufanya hivyo ni jambo jema. Lakini pamoja na elimu ya sayansi iliyotajwa hapa kuwe na uadilifu wa jambo hili, kwa sababu Afisa akishateuliwa kuwa ni Afisa asiende tu kwa uafisa wake lazima afikie malengo yaliyokusudiwa. Hili litakuwa ni jambo jema sana kwa sababu ukitoka kwa kujigamba kwamba mimi ni Afisa na ukabaki basi jambo lile haliwi nzuri hata siku moja, lakini ukifuatilia katika majukumu uliyopangiwa ukawa unaangalia jambo lile utafanikisha na litakuwa zuri sana.

Mhe. Spika, faida ya kutungwa mazingira ni faida nzuri sana. Kwa mfano nitoe mfano wa kijiji changu cha Kojani kisiwa kule Kojani ndani ya jimbo langu. Kule tuna msitu ulioitwa Kikwajuni, basi msitu ule huruhusiwi kukata hata mti mmoja.

Lakini tulipowauliza wazee wetu kwa sababu gani hukati mti pale, wanakwambia kwamba hii inasaidia hata inapokuja dharuba ya upepo basi ni kinga yetu. Kwa hivyo kutunza mazingira ni jambo zuri sana. Lakini tu niseme katika maafisa hawa kuna mambo mbali mbali hata wananchi wanapokwenda katika sehemu ya vituo vya hospitali, pale ni sehemu ya mazingira kwa sababu wananchi wanasubiri mazingira pale ya afya na watu ni wengi wana maradhi mbali mbali.

Lakini inasikitisha sana kama maafisa wetu hawa wanachelewa au wahudumu wanachelewa kuingia kazini, jambo ambalo mkusanyiko wa watu pale ni wengi na wana matatizo mbali mbali. Wananchi wanajitahidi kutoka mbali kwenda katika sehemu ya afya, mambo haya yapo vijijini na mijini.

Lakini mimi nimeshuhudia pale kwenye Hospitali ya Chake-Chake kwamba watoa huduma wanachelewa. Kwa mujibu wa nchi yetu hii nafikiri kuingia kazini ni saa moja na nusu na mpaka saa mbili mambo yote yameshakaa sawa, lakini inafikia saa tatu au saa nne siku nyengine daktari hajaingia kuhudumia wagonjwa. Kwa hivyo mkusanyiko ule wa watu unaweza ukaleta matatizo ya afya na mazingira. Mhe. Spika, maafisa hawa watakapoteuliwa, hiyo hali ni jambo moja ambalo walisimamie kwa nguvu zao zote.

Mhe. Spika, maafisa hawa wanapoteuliwa basi wakubali kufanya kazi na jamii. Kama nilivyoeleza kumpongeza Mustafa Aboud Jumbe na hawa wakikubali kufanya kazi na jamii basi mafanikio yapatikana vizuri sana.

Halafu kuwepo na tathmini ya kikazi kila mara basi kutaleta ufanisi mzuri sana. Vile vile kuwepo na afisi na zisiwe mjini tu mpaka na vijijini viziwepo kwa sababu mambo haya huja katika miji tu, lakini na vijiji huko ndiko kwenye mazingira machafu zaidi.

Mhe. Spika, vile vile kutolewe vitendea kazi katika hali hii ya afya na mazingira basi wale wanaofanya mazingira ya usafi wanakuwa na wakati mgumu kwa kukosa vitendea kazi. Mtu anakwenda kufanya usafi lakini hata *gloves* za kuvaa, hana viatu, anafanya kazi kwa kutumia mazoea tu. Kwa hivyo hilo ni jambo ambalo lichukuliwe na kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, haitoshi na jambo kubwa hasa kwa jamii ni elimu. Elimu ikiwafikia wananchi basi ni wepesi sana maafisa wetu hawa kazi zao zitakuwa ni rahisi sana. Kuwe na mdahalo wa mara kwa mara na semina ya kuwafahamisha watu waelewe namna gani ya mazingira na afya.

Mhe. Spika, leo nilisema mchango wangu sio mkubwa lakini tu katika hitimisho langu, naomba nitoe nasaha ndani ya Baraza lako tukufu. Mhe. Spika, Baraza hili ni la wananchi na kwamba Baraza hili ni la wananchi basi wananchi wetu wanatuangalia humu tunafanya nini wanaotuwakilisha sisi mpaka tukawa ni wawakilishi na kuwakilisha wao.

Baraza hili limepata sifa nyingi ndani ya Zanzibar na nje ya Zanzibar, na tunapata wageni mbali mbali wakiwepo pale juu kuja kuangalia namna ya Baraza linavyokwenda. Lakini hivi sasa kunakuwa na mwelekeo ambao unaotaka kuturejesha kule kule. Kwa hivyo nawanasihi sana Wajumbe wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi tuangalie nini walichotutuma wananchi, hoja yetu sisi si malumbano ndani ya Baraza hili, hoja ni kuwakilisha wananchi vizuri ili wapate shughuli za maendeleo. Tukirudia katika mijadala ya kuvutana hatuna chochote Baraza hili litashuka hadhi na mengi hayatofanikiwa katika shughuli za maendeleo.

Mhe. Spika, kwa haya machache nasema ahsante sana.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kupata fursa ya kusema machache katika sheria iliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, inavyoelekea Baraza lako mara hii linaingia usajili. Ni jana tu tulimaliza ile sheria ya usajili wa wakaazi lakini na hii sheria tunayotaka kuipitisha leo pia imefanana na ile ya jana kwamba tunataka kushughulikia usajili na baadae kuwapa leseni.

Mhe. Spika, kwa ujumla sheria hii ni nzuri na tunatarajia itakapokuwa *affective* matunda yake tutayaona. Na imani yetu kwamba tumo katika karne nyengine, kwa hivyo tunataka tuione nchi yetu ina *move forward* angalau *one step* tusibakie tu pale tulipoachia na wana mapinduzi.

Mhe. Spika, sasa niende kidogo mswada wenyewe. Mhe. Spika, ukiangalia kifungu cha 33, kinasema kwamba endapo mtu aliyepokea wito wa Baraza wa kwenda kutoa ushahidi na kuwasilisha nyaraka. Mimi nafikiri hapa kwanza hawa watu tungeliwafanya wawili; tukamfanya kwamba huyu mtu aliyepokea ushahidi akawa yeye yupo mbali, halafu labda tukawa na mwengine aliyepata wito wa kwenda kutoa ushahidi na kupeleka nyaraka, kwa nini ninasema hivyo.

Mhe. Spika, kwa sababu huyu aliyekuwa anapeleka ushahidi tu yeye pengine anatakiwa kutoa ushahidi tu na ana hiyari yake akasema mimi ninataka kwenda au sitaki kwenda. Lakini huyu ambaye atakuwa yeye anawasilisha na nyaraka hatoweza kupinga kwa sababu inawezekana kwamba zile nyaraka aliwahi kupewa huko nyuma. Kwa hivyo yeye akatakiwa aziwasilishe. Kwa hivyo ushahidi wa kuziwasilisha utakuwa upo, hivyo akikataa anaweza akatiwa katika hatia lakini huyu mwengine wa kwamba yeye anatakiwa akatoa ushahidi tu, basi yeye anaweza akakataa tu moja kwa moja kwa sababu hakuna jambo ambalo linalomlazimisha akatoe ushahidi.

Sasa ningependa tu kifungu hiki kikatofautishwa. Lakini pia katika kifungu hiki kuna kifungu (a) atashindwa bila ya sababu ya msingi kuitikia wito au kifungu (b) atakataa bila ya sababu ya msingi kujibu masuala aliyoulizwa.

Mimi nafikiri watu hawa na watu hawa waliotajwa kifungu (c) atafunga shughuli za Baraza na atamkejeli mjumbe wa Baraza tukawapa adhabu tofauti. Tusingewapa adhabu ya aina moja, kwa sababu hawa wa juu ninahisi makosa yao ni madogo ukilinganisha na hawa ambao wametajwa hapa chini.

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye kifungu cha 20. Kama nilivyosema mwanzo kama jana tulikuwa tunapitisha sheria za usajili wa Wazanzibari. Nikiangalia sheria hii kifungu cha 20 kinasema “Kila mgeni”. Sasa sijui katika awamu tunayokwenda mbele katika nchi hii tutakuwa tuna mgeni, kwa sababu ninahisi sasa tutakuwa tuna Wazanzibari ambao watabaguka tu; watakuwa wengine ni wakaazi na wengine watakuwa wana sifa nyengine. Lakini haitokuwa busara sasa hawa watu tukawaita wageni kwa sababu sheria tayari tumeshapitisha kwamba sasa tutawasajili na hawa wageni tutawapa jina lao. Sasa sijui tukiweka kipengele hiki cha kwamba kila mgeni anayetaka kufanya usajili tutakuwa tuna uhalali wa sheria hii au laa.

Lakini jengine Mhe. Spika, katika kifungu cha 18 tunasema kwamba kila ombi la usajili wa leseni litaambatanishwa na malipo. Mimi ningependa kusema kwamba haya malipo yangeidhinishwa mapema katika sheria hii. Tukasema jee malipo haya yatakuwa ni kiasi gani, kama tulivyoainisha katika adhabu kwamba atalipa kiasi gani basi na hapa pia tukasema kwamba huyu atatakiwa au malipo ya leseni hiyo kwa maafisa wa ngazi tofauti, tukaweka kiwango mapema.

Lakini jengine Mhe. Spika, katika kutoa leseni kifungu cha 21, tumesema kwamba kutakuwa na masharti maalum ya kuwa mtu apewe leseni. Lakini pia tumetoa *offer* kwamba kutakuwa na usajili wa muda. Sasa kwa nini kuwe na usajili wa muda, hili mimi ndio najiuliza wakati bila ya kutimiza masharti huwezi ukapewa hii leseni mpaka uwe umetimiza yale masharti yake ndio upewe leseni yenyewe.

Sasa vipi tena tumpe mtu usajili wa muda na yeye atakuwa pengine hayo masharti hatujui kayatimiza au hajayatimiza. Nafikiri mimi kama tunatoa leseni tusubiri mtu atimize masharti yake ili tumpe leseni. Haya mambo ya kusema kwamba tumpe usajili wa muda tuyaondoe kabisa. Nafikiri Mhe. Spika, na mimi niseme kwamba kwa vile madhumuni yamenitosheleza ya kuwepo sheria hii na mimi naunga mkono hoja.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, inaonekana leo Waheshimiwa hawana maneno mengi ya kusema, lakini hata mimi pia sina maneno mengi isipokuwa nataka ufafanuzi tu kidogo kwenye mswada huu.

Mhe. Spika, nilijaribu kuupitia huu mswada una mambo sio mengi, kuna maafisa wa mazingira na maafisa wa afya ya jamii, kuna Baraza la maafisa hawa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe wale waliochangia na ambao basi wakitoke nje wakumbuke kwamba shughuli hii huenda ikamalizika muda mkubwa ujao. Kwa hivyo niwaombe wale wote walioko nje basi waingie ndani tuimalize kazi hii kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, nasema nilikuwa naendelea na mambo niliyoyaona humu ambayo si mengi ninasema.

Sasa kuna Baraza la maafisa hawa wa mazingira na afya, kuna mrajis, baada ya hapo nilichokiona kuna usajili na leseni pamoja na malipo ya usajili na malipo ya leseni, baada ya hapo kuna makosa na adhabu.

Sasa ukisoma madhumuni unakuta hawa maafisa walikuwepo labda labda mswada huu lengo lake ni kuwafanya rasmi, maana yake ni kuwasajili na kuwatambua ndio madhumuni ya huu mswada.

Sasa bahati mbaya mimi kuna mambo ndio nikasema nipate ufafanuzi kidogo kwa sababu ukitaka maafisa wa afya, mimi siwajui na siwajui kwa sababu afya ni jambo pana na nilidhani maafisa hawa ni hawa waliomo mitaani mwetu. Kwa mfano kuna watu maafisa wa afya lakini wa wanyama na wanashughulikia wanyama tu, wale madaktari wa wanyama, nilifikiria pengine ndio wale.

Lakini mara nyengine nikafikiria labda humu katika mitaa yetu pia kuna akinamama fulani huwa wanatoa huduma hasa za kujifungua, tunawaita wakunga mimi nikafikiria labda ndio wale, maana yake siwajui.

Lakini nilipokuwa ninasoma kifungu cha 17, kuna sifa walizoekewa hawa. Kumbe ni watu wakubwa sana. Maana yake mtu anakuwa na shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu itakuwa ni mtu mkubwa kumbe sio hawa niliokuwa ninafikiria mimi.

Lakini sasa ikiwa ni watu wa aina hii labda itakuwa wapo hospitali sasa na ikiwa wapo hospitali maana yake nini, maana yake ni watu wanaendelea kuwa wapo. Sasa jee lengo ni kuwapa leseni madaktari au vipi. Naomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri anifahamisha maafisa wa afya ni akina nani, mimi siwajui.

Lakini pia kwenye mswada huu haukutaja kazi zao rasmi. Maana yake kama wangetaja zile kazi alau tungejua kumbe ni akina fulani lakini huu mswada haukutaja kazi zao. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri aje anifahamisha hawa ni akina nani na kazi zao hasa ni zipi.

Haya mengine sina matatizo nayo Mhe. Spika, kwa sababu yapo wazi, kuna Baraza lipo wazi limeelezwa humu na kazi zake, Mrajis na kazi zake sina tatizo nazo. Lakini nilikuwa naangalia kidogo makosa nafikiri ya kiuandishi. Mhe. Spika, niliwahi kutoa maelezo juzi kwamba wenzetu hawa wanaotunga basi makosa madogo madogo kama haya wangekuwa wanayaangalia mapema, kwa sababu chombo hiki ni kikubwa na miswada yote takriban kabla ya kufika hapa Barazani inapita kwa watu walio makini sana na walio na uwezo mkubwa sana wa kuandika kuliko sisi hapa tuliopo. Kwa hivyo, kuna mambo yanajitokeza ambayo hayaleti sura nzuri na nimeyagundua hapa kwenye kifungu cha 4(c), ambacho kinasema;

Kifungu cha 4(c)

"Mkurugenzi mwenye dhamana ya afya ya mazingira".

Aah! Hii haina matatizo nafikiri nilikuwa sijaisoma vizuri. Lakini ukisoma kifungu cha 4(d) ambacho kinasema;

Kifungu cha 4(d)

"Mwakilishi kutoka wizara yenye dhamana na tawala za mikoa".

Nadhani sio Kiswahili sahihi. Mwakilishi kutoka wizara yenye dhamana na tawala za mikoa, au yenye dhamana ya tawala za mikoa. Ni kosa la kiuandishi, lakini sasa linaweza likabadilisha maana kwa sababu hii ni sheria na sheria kila neno moja linakuwa na maana nyengine pengine.

Ukienda mbele kwenye kifungu hicho hicho kwenye ule mstari wa tatu, pale kuna Waziri mwenye dhanama, imejirudia vile vile tena. Waziri mwenye dhamana na tawala za mikoa au dhamana ya tawala za mikoa. Nilikuwa nahisi dhamana ya tawala za mikoa ndio sahihi.

Pia nilitaka niongeze kidogo kwenye hicho kifungu cha 4(1) (a), yule Mwenyekiti wa Baraza, ameelezwa pale kwamba ni mwenyekiti ambaye atakuwa na uzoefu wa mambo ya afya. Mimi nilikuwa naomba isiwe uzoefu tu, kwa sababu kama Afisa wa Afya anakuwa na sifa na shahada maalum basi na huyu Mwenyekiti ni vyema akawa na sifa maalum ambazo mswada huu hazikumueleza, wamesema uzoefu tu. Sasa ikiwa yeye ni mzoefu lakini anaongoza watu wenye taaluma zao kubwa, nafikiri anaweza kushindwa kuwaongoza. Kwa hivyo nilitaka na huyu Mwenyekiti na yeye awe na sifa, japo na uzoefu utakuwepo, lakini kwanza awe na sifa.

Halafu kifungu cha 11 kuna maoni ya Baraza, kinasema;

Kifungu cha 11

"Maamuzi yoyote ya Baraza yataamuliwa kwa uchache wa kura".

Nadhani itakuwa imeandikwa kimakosa. Ilivyotakiwa iwe kwa wingi wa kura, angalau hivyo labda. Sasa naomba yafanywe marekebisho hayo. Nafikiri Mhe. Spika, baada ya hayo machache kama nilivyosema na mimi sina maneno mengi, nilitaka Mhe. Waziri zaidi anipe ufafanuzi ili niwajue hawa maafisa wa afya na kazi zao zaidi. Baada ya kusema hayo na mimi naunga mkono mswada huu pamoja na wananchi wangu. Ahsante.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, sinabudi kwanza kumshukuru *Allah Subhanahu Wataallah* na kumtakia Rehma Mtume wetu Muhammad (SAW), kwa asubuhi hii kupata nafasi adhimu na mimi kutoa mchango wangu katika mswada huu wa sheria ya usajili na usimamizi wa maafisa wa afya ya jamii na mazingira na kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na uongozi wake kwa kuliona hili kwamba nchi yetu inaingia katika tatizo la uharibifu wa mazingira. Kwa hivyo, wakaona kwamba sasa hatuna budi kuuleta mswada huu ili kuwekewa sheria ya mambo haya. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mchango wangu leo utakuwa katika sehemu ya pili ya kuanzishwa kwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira.

Mhe. Spika, baada ya shukrani zangu niseme kwamba nchi yetu kwa muda mrefu inaendelea kuwa na vyombo ambavyo vimeishiwa na wakati. Mhe. Spika, hapa Zanzibar tuna magari ya toka nitoke, yanapotembea barabarani

kwa kweli yanachafua hali ya hewa na mazingira ya mji wetu na maeneo yetu mengine. Kwa kweli hili ni tatizo magari haya yamekwisha, magari haya kwa kweli yafanywe kwamba hayana tena wakati wa kupita tena katika mabarabara hasa yale ambayo majengo ya wananchi yameshikana. Kwa kweli ukipita maeneo ya Mji Mkongwe ni sehemu ambazo majumba yake yameshikana na magari kama haya yanapita katika maeneo yale, hivyo yanasababisha sana watu kupata kuumwa na mafua na maradhi mengine. Kwa hivyo, kuwepo kwa Baraza hili nahisi kwamba itatusaidia katika kupambana na vyombo hivi ambavyo vimepitwa na wakati.

Aidha, ujenzi holela wa viwanda katika makaazi ya watu. Tukichukua mfano Mhe. Spika, kama Kiwanda cha Makonyo kilichopo pale Wawi. Ni kweli kwamba wakati kilipojengwa kiwanda kile ilikuwa hali ya mazingira inaruhusu, lakini kutokana na watu kuongezeka basi kile kiwanda kiko katikati ya Jimbo lile la Wawi. Lakini ukitaka kufaidi Mhe. Spika, basi upite wakati kiwanda kinazalisha na hali ya hewa imefanya gugu la wingu. Moshi ule wote unaingia katika kijiji kile na barabara utafikiri kwamba wananchi wanashughulika katika mambo ya upishi kwenye majumba yao, kumbe ni moshi tu unaoingia katika maeneo ambayo wananchi wanaishi na itakuwa siku nyengine kufika hata magari kuwasha taa, kutokana na gugu lile. Kwa hivyo, kuwa na viwanda katika maeneo kama hayo kwa kweli tunaathiri hali nzima ya mazingira na kupata wananchi wetu matatizo.

Mhe. Spika, nikiendelea nije kwenye mazingira ya baharini. Ni kweli kwamba wananchi wetu wengi hasa wavuvi, uvuvi wanaovua hauendi na wakati ama kutokana na uwezo wao mdogo wanavua katika maeneo ambayo ni ya matumbawe. Inasemekana kwamba hapa Zanzibar tuna aina karibuni 400 ya matumbawe ambayo hayapatikani popote duniani isipokuwa hapa Zanzibar. Lakini kutokana na uvuvi huu basi husababisha wavuvi wetu hawa kuyavunja mazingira yale, ambapo katika mazingira yale ya matumbawe basi samaki ndio sehemu zao wanazozalia na kucheza, na hatimaye sisi tunafarijika kwa kupata vitoeleo.

Mhe. Spika, uwezo wa wananchi wetu ni mdogo, kwa hivyo ningeshauri sana serikali ikachukua hatua za makusudi ili kuhakikisha wamewawezesha wavuvi wetu hawa, wamewakopesha vyombo na vifaa vya kuweza kwenda katika bahari zenye kina, ili kunusuru mazingira ya baharini hasa sehemu za pwani.

Pia Mhe. Spika, niseme kwamba ulimaji wa kiholela na uchomaji moto wa misitu na ufuaji wa ovyo ovyo wa nyuki usiokuwa na utaalamu maalum, pia hizi ni sehemu zinazochafua sana mazingira. Kwa hivyo, mimi nashukuru sana kwa Mhe. Waziri kuunda hili baraza ambalo liwe na usimamizi wa dhati.

Mhe. Spika, tuna vyombo vingi tu tunaunda humu katika nchi yetu, lakini mtu ana ile faida ya kutangazwa kuwa yeye ni afisa na kadhalika. Lakini ufuatiliaji hatuna Wazanzibari, tukitaka tusitake hatuna ufuatiliaji. Kwa hivyo, tuendeleeni tu kuunda vyombo, tukiangalia matatizo bado yako pale pale na bado yanazidi kwenda mbele.

Kwa hivyo mimi nashukuru sana kwamba Mhe. Waziri ndiye mwenye mamlaka ya vyombo hivi. Hivyo tusibakie kama tulivyobakia huko nyuma, tuamke sasa, ili nchi iendelee basi ni kusimamia zile nyenzo ambazo tumeziweka ili ziweze kufanya kazi zake vizuri. Mhe. Spika, nakushukuru naunga mkono mswada huu. Ahsante.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu *Subhanahu Wataala*, aliyetujaalia uhai na uzima ili tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikukushukuru na wewe kwa kunipatia na mimi nafasi hii ya kutoa mchango wangu mdogo katika mswada uliopo mezani kwa wakati huu.

Mhe. Spika, nianze na kumpongeza Waziri na watendaji wake kwa kuona kwamba umefika wakati sasa wa kuleta mswada huu ili kuona wanalinda afya ya jamii ya Wazanzibari. Mhe. Spika, kwa kweli katika mswada huu wa usajili na usimamizi wa maafisa wa afya ya jamii na mazingira na kuanzisha baraza la maafisa hao wa mazingira ni jambo zuri. Mswada huu umekuja kwa sababu nyuma yake tayari tumeshapitisha sheria ambayo ni ya uhifadhi na usimamizi wa vihatarishi vya afya ya jamii na afya ya mazingira.

Mhe. Spika, mswada huu wa leo unakuja kuwapa nguvu sasa watendaji hao kuweza kutekeleza hizi kazi ambazo tuliweza kuzipitisha katika kipindi kilichopita juzi tu. Mhe. Spika, ni wazi kwamba maafisa afya walikuwa wakifanya shughuli zao, lakini hawakuwa na sheria ambayo ilikuwa inawapa nguvu kuweza kutekeleza majukumu

yao kisheria. Mara nyingi walikuwa wakikumbana na mambo mbali mbali, ambayo wakija katika misingi ya sheria yalikuwa yanawapa matatizo.

Mhe. Spika, mswada huu wa kuwepo kwa maafisa afya wa jamii na maafisa hao wakapata nafasi ya kuwahudumia wananchi ni suala jema, kwani sote tunaelewa kwamba bila ya kuongozwa afya ya jamii na wizara husika ambayo ndio yenye dhamana kuu ya kulinda na kutibu, lakini pia na kuweka kinga ya jamii ya Kizanzibari. Tunajua sote kwamba kuna mambo mbali mbali yanayofanyika katika afya ya jamii ambayo hayastahiki. Hii inazingatia kwamba kuna wafanyabiashara mbali mbali wa mambo ya vyakula. Hawa wataingia moja kwa moja kuona kwamba maafisa wake watapata kuona.

Mhe. Spika, leo sote tunashuhudia kwamba kuna sehemu mbali mbali za biashara zinazofanywa ambapo wananchi wanafanya biashara na kula, lakini hali za mazingira za hali hizo huwa haziruhusu. Mhe. Spika, huleta mashaka au tabu au kusababisha wakati mwengine hali mbaya ya kuweza kuleta maradhi ya uambukizo. Lakini maafisa hao kwa sababu walikuwa hawapo kisheria wakifanya kazi kama watu wa afya tu, basi ilikuwa mara nyingi hauonekani umuhimu wao. Ndio sababu za msingi katika lile baraza kutajwa kwamba watahusishwa na wale watu ambao wanahusika na manispaa, ili kuungana nao pamoja kuona kwamba watasimamia hali hii.

Mhe. Spika, kuna sehemu mbali mbali ambazo watu wamechimba mashimo ya makaro na kusababisha maji kuzagaa ovyo. Lakini hakukua na utaratibu maalum ambao unamgusa moja kwa moja afisa huyu, ili kuona kwamba vipi anaweza kuchukua hatua katika hali hii.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu hauna cha kuongezewa kwani ni dhahiri kwamba huu mswada umekuja kuunga nguvu juu ya ule mswada tulioupitisha juzi. Mimi ni mmoja kati ya wadau ambao tulitoa marekebisho na kuweza kuufanya vyema mswada huu na kuweza kuuleta hapa ili wenzetu waweze kuuchangia.

Mhe. Spika, niliona na mimi nisimame ili niiunge mkono hii hoja katika Baraza lako hili tukufu, kuona kwamba na mimi naunga mkono hoja hii ili kuwapa baraka hawa maafisa ambao watapata nafasi hii ili wafanye kazi zao kwa uadilifu.

Mhe. Spika, huo ndio msingi mkubwa, kwani ni mazoea kwetu kutunga sheria nyingi, lakini naomba kuwa sheria hii isimamiwe ipasavyo ili itekelezwe, kwani ukiukwaji na matumizi mabaya ya mizunguko yetu ya maisha na katika mazingira yetu kwenye jamii ni mambo ambayo yanakwenda sambamba. Pale ambapo wananchi wamezunguka kuna majaa mengi yametayarishwa na huchomwa moto, na wakati mwengine hutoa harufu ambayo pengine kwa afya ya jamii inaleta mashaka. Nadhani malengo hayo yatafanikiwa. Kuna sehemu nyengine maji machafu, makaro na wengine vyoo vyao vinaleta athari na vinapitisha maji machafu ambayo wakati mwengine watoto huenda kuchezea na kusababisha maradhi mbali mbali.

Mhe. Spika, nadhani Wizara ya Afya kwa kujua kwamba wao ndio wenye dhamana na wao ndio wenye wajibu kwa wananchi wa Zanzibar katika kuwahudumia na kutoa taaluma, lakini pia wakaona ipo haja sasa ya kutengeneza chombo hiki na maafisa hawa kuwapa baraka ili wawe na sheria maalum waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi. Kimsingi naomba sana kwamba sheria hii naamini kuwa itapitishwa, wengi tumeiridhia, lakini itakapopitishwa nimuombe Mhe. Waziri aisimamie vilivyo na kuona kwamba wale ambao watakuwa na sifa za kuwa maafisa wa afya basi wawe ndio hao na isiwe vyenginevyo, na kama itakuwa hivyo ndivyo basi naamini kwamba tutajenga mazingira mema na afya njema kwa jamii ya Kizanzibari.

Baada ya kuyasema hayo Mhe. Spika, mimi pamoja na wanawake wenzangu wa Wilaya ya Kaskazini B naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuchangia mswada huu. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 2 kinahusu kuanzishwa. Katika kifungu cha 4(1) (g) kinasema;

Kifungu cha 4(1) (g)

"Kutokana na wajumbe wawili katika sekta binafsi"

Je, Mhe. Waziri wajumbe hawa watateuliwa kutoka taasisi binafsi au taasisi gani. Mhe. Spika, Sehemu ya Tatu, sehemu hii inahusiana na usajili na utoaji wa leseni. Kifungu cha 17(2) kimetoa sifa ya mtu anayeweza kusajiliwa

Mhe. Spika: Mhe. Viwe Khamis Abdalla, nikuombe ukae kitako usubiri tufanye hii kazi.

Mhe. Asha Abdu Haji: Kifungu cha 17(2) kimetoa sifa ya mtu anayeweza kusajiliwa na kupewa leseni.

Mhe. Spika, kwa kuwa mara nyingi watu ambao hutoa leseni kwa usajili huwa na urasimu mkubwa sana, licha ya kwamba muombaji huwa na sifa husika mara nyingi au sio zote, kama hii huonekana kwamba anapata usumbufu japokuwa ana sifa. Mhe. Spika, huwa na usumbufu mkubwa kwa muombaji ambaye hutokwa na imani na kuchoka kwa chombo au taasisi husika, lakini pia hata serikali yenyewe.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri awatanabahishe Wajumbe wa Baraza ili kufanya kazi, wasije kuipa kikwazo na kuifanyia ukiukwaji na utekelezaji wa sheria hii. Mhe. Spika, maafisa wa afya ya jamii ni vyema ikiwa wanaishi katika jamii zao wanazotoka, ili kazi ifanyike inavyopangwa kwa utekelezaji na ufanisi mkubwa katika kazi zao.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuishi nje ya jamii zao kutasababisha usumbufu na kutokuwa na utekelezaji kwa kazi hiyo ya mazingira. Mhe. Spika, kwa hivyo ni jambo la busara kupangiwa na kuishi katika jamii husika. Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu.

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, kanuni ya 71, naomba ninukuu hapa mara kabla ya uamuzi wowote kufanyika, ikiwa Mjumbe yeyote aliyehudhuria atapinga kwa kudai kwamba mbali ya Spika, Wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote, basi kama Spika, atathibitisha kuwa wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote, basi atasimamisha shughuli kwa muda wa dakika tano na huku muhudumu kwa maelekezo ya Katibu, atapiga kengele kwa vituo, yaani sio mfululizo.

Mhe. Spika, kwa kifupi *quorum* haitimii Barazani na kwa mujibu wa kanuni hii, naomba sana Baraza lako uliakhirishe ili wahudumu wapate kuwatafuta Wajumbe wengine waje humu ndani. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wakati mjadala unaendelea acha niwaamuru watendaji wapige kengele ili wajumbe wengine waingie na mjadala uendelee. Mhe. Salim Abdallah Hamad endelea. Halafu wahudumu pigeni kengele ili kuwaita Waheshimiwa Wajumbe waingie ndani.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu mdogo kabisa katika mswada huu wa sheria ya usajili na usimamizi wa maafisa wa afya ya jamii na mazingira na kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza kwa kupitia Serikali yetu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa, nitoe shukrani kwa kuuleta mswada huu muhimu ambao unamgusa binadamu na mazingira yake moja kwa moja.

Mhe. Spika, katika mswada huu katika ukurasa wa 84 chini hapa, imeelezwa kuwa huduma za afya ya mazingira, maana yake ni huduma zinazotolewa kuhusiana na karo za maji machafu, takataka, wadudu waharibifu, usafi wa chakula, usafi wa maeneo, kinga ya afya ya jamii na shughuli nyengine zinazohusiana na hayo. Ni kisehemu kidogo lakini chenye maelezo makubwa sana.

Mimi Mhe. Spika, labda ningemuomba Mhe. Waziri anisaidie tu, kuwa kumeundwa. Baraza hili lakini kuna mambo ambayo tokea zamani yanaleta uharibifu wa mazingira yameshaanza na mengine yanaendelea ufafanuzi wake katika kuyaondoa.

Kwa mfano, Mhe. Spika, nyumba zetu zina makaro ambayo yanachukua maji machafu na kadhalika, utaratibu mkubwa tulionao hivi sasa uchafu ule unamalizikia baharini. Baharini ni sehemu ambayo kuna viumbe vinavyoishi na ni chakula cha binadamu, na pengine wanaweza kutumia uchafu ule kama ikiwa ni chakula chao, kwa bahati mbaya ikawa inawezekana pengine wanaweza pia baadhi ya uchafu uliomo ni wenye kuleta dhara kwa sisi tunaotumia samaki wale.

Kwa kuwa suala hili limeanza tokea zamani na linaendelea na ni lenye kuchafua mazingira ya bahari. Kwa hivyo, sijui Mhe. Waziri kwa kutumia hilo Baraza lake atakuwa na mpango gani wa kuweka njia nyengine ya miundo minu ya kugida maji haya machafu na takataka yasiingie mwahala ambapo yatasababisha uharibifu kwa upande mwengine.

Jambo la pili Mhe. Spika, kuna wadudu hawa waharibufu. Lakini ninavyojua katika dunia Mwenyezi Mungu ameumba mambo na viumbe alivyoviumba wanategemeana na kila mmoja ana faida kwa mwenzake, basi mmoja akitoweka kuna hasara pale inatokea na hivyo mfumo mzima wa maisha unakuwa na matatizo.

Kwa mfano, kunguru ni wanyama waharibifu na hawa tunawaangamiza na tunaendelea kuwaangamiza, lakini kwa vyovyote vile wanayo faida kubwa sana, kama vile masuala ya kuondoa uchafu katika mazingira, pia kuondoa wadudu wanaoharibu kilimo na kadhalika vile vile ni waharibifu. Sasa kuondolewa kwao kuna mambo ambayo inabidi lazima kuwe na kitu cha kujaza, ili hali ya maisha ipatikane vile vile.

Kwa hivyo, kila wale wadudu waharibifu wakishaondolewa wenye mfumo kama huu, je wizara ina mpango gani wa kufanya *replacement*, ili *ecosystem* isiweze kubadilika.

Mhe. Spika, kwa sababu ya maendeleo ya binadamu kuna mambo yanafanyika na yanapofanyika yanaleta dhara. Kwa mfano, kiwanda ni sehemu moja ya maendeleo na hivyo hivyo viwanda vyetu vidogo vidogo tulivyonavyo, basi vingi viwanda hivyo katika kuwekwa kwake hakukutiliwa maanani au indhari kuhusu usafi wa mazingira, na hivi sasa tunaharibu mazingira ya hali ya hewa pamoja na viumbe wanaotumia hewa ile.

Kwa kweli mfano mkubwa ni kile Kiwanda cha Makonyo kilichopo Chake Chake, lakini pia ile njia ya barabara mpya kwenye kile Kiwanda cha Mpira na ile harufu inayotoka ya mipira ni mbaya sana kiasi ambacho inatisha na kuna watu wanaoishi katika sehemu ile.

Sasa mambo haya tayari yapo tokea zamani, sijui Mhe. Waziri atakuwa na maelekezo gani ikiwa sababu ni kuondoa haya matatizo, lakini yapo kwa faida ya binadamu yataondoka na shughuli zetu za maendeleo ziweze kuendelea.

Mhe. Spika, kuhusu kitu muhimu duniani ni hewa, sisi tunavuta hewa ikiwemo *oxygen* ambayo inayotupa uhai, miti inavuta hewa ikiwemo *carbon dioxide* inayoipa uhai miti na tunabadilishana hewa baina ya binadamu na miti.

Kwa hivyo, kutokana na maisha ya binadamu kuna huu mtindo ambao ni mbaya sana wa kukata miti ovyo, kwa sababu ukikata miti ovyo unasababisha mambo mengi sana. Kwanza ardhi kuwa kavu, mmong'onyoko wa ardhi na isitoshe miti inasaidia kuleta rutba katika ardhi, pia miti inasaidia kusafisha hewa kwa kutumia ile *carbon dioxide*, na miti ikiondoka ina maana hewa chafu itakuwepo kwa wingi.

Vile vile si hilo tu Mwenyezi Mungu amejaalia kuna viumbe ambao si miti ni wanyama ambao wanaishi kwenye miti na wana faida kubwa sana. Kwa mfano, popo wana faida juu ya kusambaza mbegu katika ardhi na kueneza misitu yetu na wanyama wengine kama hao.

Kwa bahati mbaya binadamu wanaikata miti ovyo na wanaleta hasara kubwa sana kwa sisi viumbe tunaohitaji miti kwa kupata hewa safi, ardhi inayohitaji miti kwa kupata rutba pamoja na wanyama wanaopata chakula chao kwenye miti na kuweza kueneza misitu ambapo ni jambo la muhimu sana. Kwa kweli kazi hii inaendelea miaka yote na kuendelea kwake ni hatari ndio tukafika hapa tulipo.

Mhe. Spika, kwa upande huu wizara inajipanga vipi kuona kuwa pamoja na kuwa miti itakuwa inaendelea kukatwa, lakini kunakuwa na *replacement* au uwakilishi wa miti mingine, ili hali isiende kama inavyokwenda sasa.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba mimi naomba kupata maelekezo tu. Kwa hayo, machache nashukuru kwa kunipa nafasi hii na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mswada wa Usajili na Usimamizi wa Maafisa Afya ya Jamii pamoja na Mazingira.

Mhe. Spika, mswada huu umekuja wakati muafaka, kwani uharibifu wa mazingira umekuwa mkubwa. Kwa kweli mazingira yetu ya ardhi, bahari na hewa yamekuwa yakiendelea kuathirika siku hadi siku. Hali hii ilitokana na kutowepo kwa chombo madhubuti cha kusimamia mazingira yetu. Kwa hiyo, mswada huu umekuja wakati muafaka na utakuwa ni mkombozi wa mazingira yetu.

Vile vile kilimo kisichokuwa na utaalamu huwa kinaharibu mazingira. Mhe. Spika, suala la kuleta magari chakavu kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakiongeza hewa ukaa pamoja na kuleta athari ya mabadiliko ya tabia nchi. Kwa hivyo, Mhe. Spika mswada huu umekuja wakati muafaka na utaokoa mazingira yetu pamoja na kutusaidia hata sisi tunaoishi katika mazingira hayo.

Katika mswada huu nimeona wasaidizi wa maafisa wanatakiwa wawe na kiwango cha elimu ya *diploma*, hii ni nzuri sana na itatusaidia. Lakini naiomba serikali Mhe. Spika na wale waliokuwa hawana kiwango cha elimu hii, basi serikali iwasaidie kuwaendeleza ili na wao wafikie kiwango hichi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi hii kuwepo katika majukumu yetu ya kila siku ambayo tumetumwa na wananchi wetu wa Zanzibar.

Pili nachukua nafasi ya kukushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia angalau kwa muhtasari Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na Kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Vile vile nimpongeze sana Mhe. Waziri kutuletea mswada huu muhimu. Mhe. Spika, tukitaja neno mazingira kwa kweli lina uwanja mpana sana, kwa sababu tunaishi ndani ya mazingira hayo, hatuna budi ila mazingira yetu yawe katika hali ya usafi na uzuri. Kwa hivyo, naipongeza Wizara ya Afya chini ya Mhe. Waziri Juma Duni Haji kuanzisha mswada huu, kwa ajili ya kuikomboa Zanzibar katika mazingira yasiyofaa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mchango wangu nataka niende kwenye sehemu ya pili ya kuanzishwa na Baraza la Mswada huu kifungu cha 4(1) (a) Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 4(1) (a) kinaeleza hivi:-

> "Mwenyekiti ambaye atakuwa na uzoefu wa mambo ya afya ya jamii na mazingira na mambo ya afya na atateuliwa na Waziri".

Kwa kweli hii ni *point* muhimu sana, lakini namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho, anieleze tu pamoja na uzoefu wa afya je Mwenyekiti huyu angekuwa na kiwango gani cha elimu, kwa sababu Mwenyekiti ni mtu mkubwa kiasi pangekuwa na kiwango maalum cha elimu akakitangaza hapa, basi lingekuwa ni jambo zuri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atueleze kwamba Mwenyekiti angalau angekuwa na kiwango gani cha elimu.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye kifungu cha 17 sehemu ya tatu katika usajili na utoaji wa leseni, Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 17(2) (a) kinaeleza hivi:-

> “Kuwa afisa wa afya ya mazingira awe na shahada ya kwanza au ya juu inayoonesha kwamba amefaulu mafunzo ya afya ya sayansi ya mazingira au fani nyengine inayolingana au inayothibitishwa na Baraza”.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho, anieleze je hivi sasa watu wenye sifa hii wapo.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huu mfupi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na Kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea mswada huu katika Baraza hili letu tukufu, ambalo litatuongoza katika kutenda shughuli zetu hizi.

Lakini katika kutenda kazi niseme kwamba sheria hii ambayo itawapa muongozo watendaji wake wote pamoja na jamii yote kwa jumla.

Vile vile nataka niwape indhari watendaji au maafisa wote, ili kuifuata sheria hii kama ilivyotungwa, kwa sababu Mhe. Spika tukitoka nje huko hawa wananchi wetu wote huwa wanaijua sheria kuliko hata sisi tuliyoitunga humu Barazani, wanatuambia kwamba sheria mnazitunga na wala hamuzifuati. Kwa hiyo, naomba Mhe. Spika sheria hii ifuatwe kama ilivyotungwa.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 21 kifungu cha 1(a) Baraza litajiridhisha. Kwa hiyo, hapa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anifahamishe kwamba Baraza litajiridhisha au Baraza litaridhika kuwa muombaji.

Mhe. Spika, niende kwenye kifungu cha 35(1). Kwa hivyo, hii namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja anifahamishe vizuri, kwa sababu bado sijaelewa vizuri hichi kifungu kinavyoeleza, naomba kunukuu Mhe. Spika.

Kifungu cha 35(1) kinaeleza hivi:-

> “Endapo Mrajis atakuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa mtu yeyote au taasisi yoyote inatenda kosa au imetenda kosa chini ya Sheria hii au Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, anaweza kutoa taarifa ya maandishi kwa muhusika kumpa nafasi ya kulipa faini badala ya mashtaka, na hakuna mashtaka yatakayofunguliwa dhidi ya mtu au taasisi iliyolipa faini, kwa mujibu wa kifungu hichi kabla ya kumalizika kwa siku saba tokea siku ya kutolewa taarifa au tokea siku iliyoanza mashtaka au lolote katika matukio hayo lililotokea mwanzo.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aje anifahamishe, kwa sababu kwa uoni wangu nimeona kwamba hatuoni kuwa mtu anaweza kutenda kosa kwa makusudi na akajua kuwa hatachukuliwa hatua na badala yake atalipa faini. Sasa hivi hatuoni kuwa tunawakaribisha wengine na wao kutenda kosa lile, kuona hatashtakiwa na badala yake atalipa faini. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja hapa anifahamishe vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba na mimi nitoe mchango wangu kwa ufupi, ili niweze kutia baraka kwenye mswada huu.

Naomba nianze moja kwa moja mchango wangu kwenye sehemu ya pili kuhusu tafsiri. Mhe. Spika, kwenye mswada huu lilitumika neno mgeni na kwa bahati mbaya kwenye mswada ikawa halina tafsiri, kwa hivyo Kamati yangu ilipendekeza kwamba mgeni kwa mswada huyu ni yule afisa wa afya au mazingira ambaye atatoka nje ya Tanzania.

Tuliliona hilo kwa sababu kuna maafisa wa afya ya jamii na mazingira ambao wanaingia hapa kama wageni, na hawa wengi wanafanya kazi katika taasisi za kibiashara kama vile mahoteli. Kwa hivyo, tukasema kwamba kwa kuwa wizara inawapa vibali, tukaona kuna haja ya kutafsiri neno mgeni, ili huyu afisa kutoka nje ya nchi ambaye pengine ataajiriwa na kampuni fulani au mahoteli, basi iwe ni sehemu ya afisa wa afya ambaye sheria hii inamtambua.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningelichangia ni kifungu cha 7(2) na (3) Kamati yangu iliona kuna haja ya kukifuta, kwa sababu mswada huu ulipendekeza kwamba Baraza hili litoe mitaala kwa wale maafisa au vyuo vinavyotaka kusomesha afya ya jamii na mazingira.

Lakini tukaona kwamba vyombo ambavyo vinatoa mitaala na kutambua ni Baraza la Mitihani (*NECTA*), kwa hivyo si busara kwamba Baraza la Afya ya Jamii na Mazingira wao tuwape nafasi ya kutoa mitaala jambo ambalo si chombo ambacho kinakubalika katika elimu ya juu. Kwa hivyo, tunaona vifungu hivi vya 7(2) na (3) tuvifute kwa msingi huo.

Jengine ambalo tulifuta ni kifungu cha 10 na naomba kunukuu Mhe. Spika.

Kifungu cha 10 kinaeleza hivi:-

> "Endapo Mjumbe wa Baraza kwa nafasi yake, atashindwa kwa sababu yoyote kuhudhuria kikao cha Baraza anaweza kuwakilishwa na mtu mwengine kutoka katika taasisi yake.

Mhe. Spika, tumeona tufute kifungu hichi kwa sababu tumegundua kwamba baadhi ya watu wanapopewa nafasi hii wanakuwa hawahudhurii vikao, kwa sababu wanaweza kutoa nafasi ya kuwakilisha. Kwa hivyo, tulisema kwamba lazima mjumbe aliyechaguliwa ndiye mwenye kuwasilisha vikao vile, ili kuwabana, utaratibu ule kwamba usipohudhuria mara tatu basi iwe tayari umejitoa mwenyewe. Sasa kutoa nafasi kwamba mtu atoe nafasi ya kukaimu maana yake watu wengine wanakwepa kufanya wajibu wao.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka niliguse na nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba kifungu cha 4(1) kuna uteuzi wa Mwenyekiti na mswada hapa haukuzitaja sifa za Mwenyekiti kama Mhe. Mohammed Mbwana Hamad alivyozungumza.

Lakini Kamati yangu iliona busara kwamba mbali ya uzoefu wa taaluma ya afya, tukasema awe na elimu isiyopungua stashahada. Kwa hivyo, Kamati yangu iliona kwamba Mwenyekiti huyu wa Baraza hili awe na elimu isiyopungua stashahada, ili aweze kuendesha vizuri vikao vya Kamati husika.

Jambo la mwisho kabisa ambalo nataka nipate ufafanuzi ni sehemu ya sita kifungu cha 36 kuna suala zima la chanzo cha fedha. Mhe. Spika, sina wasi wasi sana na vyanzo vya fedha, lakini nina wasi wasi na naomba nipate ufafanuzi na pengine hata Mhe. Mwanasheria Mkuu anisaidie, utaratibu wa kuweka zawadi kama ni chanzo cha fedha.

Mhe. Spika nadhani umepitwa na wakati, kwa sababu watu wasio waaminifu wanachukua nafasi hii ya kupokea zawadi na hatimaye inachangia katika kudumaza maendeleo, maana yake inakuwa ni sehemu ya rushwa.

Kwa hivyo, kwa mawazo yangu nafikiri chanzo cha fedha iwe ni michango na ruzuku, lakini zawadi ambazo Baraza litapokea kutoka kwa watu binafsi nadhani tungeifuta kwa sababu inatoa mwanya kuwafanya watu ambao sio waaminifu kupokea mambo ambayo si ya msingi, na hatimaye kutuharibia sheria na utawala wetu hapa ndani.

Kwa maana hiyo, nadhani zawadi kwa Baraza hili basi tusitoe mwanya, isipokuwa chanzo iwe ni fedha kutoka Baraza la Wawakilishi au serikalini michango na ruzuku, lakini hii zawadi nafikiri Mhe. Mwanasheria Mkuu utusaidie, kwa sababu nadhani kidogo inaleta picha ambayo si nzuri na inaweza kuchochea wale ambao sio waaminifu kufanya mambo ambayo si ya msingi.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kifungu cha 36(2) mabaraza mengi hasa ya Wizara ya Afya fedha ambazo wamezitenga. Kwa mfano, kuna Baraza la Tiba Asili fedha ambazo wanazoingiziwa zinadhibitiwa na *account* yenyewe ya wizara, jambo ambalo huleta usumbufu kwenye mabaraza yenyewe. Kwa hivyo, tumegundua kwamba mabaraza haya yanakosa kufanya vikao vyao hata vile sheria imetaka.

Kwa maana hiyo, Kamati yangu ikasema kwamba fedha hizi za Baraza hili la Wataalamu wa Afya, basi fedha zote ziingie kwenye *account* yao wenyewe na ndio maana Kamati yangu ikasema kwamba kifungu cha 36(2), lazima kuongezwe maneno kwamba zitaingizwa katika *account* ya Baraza, fedha hizi zisibakie kwenye *account* ya wizara, ili kuondosha usumbufu kwa Baraza na waweze kufanya kazi zao kama inavyotakiwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono mswada huu. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na Kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na mambo mengi yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza napenda nimshukuru Mhe. Waziri kwa mswada wake huu alioutoa, ambao ni mswada muhimu kwa wananchi na wizara kwa jumla. Vile vile niwashukuru watendaji wake wa wizara hii kwa kuupanga vizuri huu mswada na sisi tukaweza kutoa mchango wetu katika masuala ya afya ya jamii pamoja na mazingira yao.

Mhe. Spika, inaonesha kuwa wizara hii ina nia nzuri katika kuwasaidia wananchi. Lakini inawezekana kwamba wizara itajitahidi katika kuweka haya kama tunayaona na sisi tunayazungumza, lakini ikawa utekelezaji wa mambo haya yasiwe mazuri sana, kwa sababu inahitaji wizara kujipanga vizuri kabla ya utendaji wa mambo haya.

Sisi sote tuliopo hapa tunaamini kwamba humo tunamoishi katika nyumba zetu pamoja na mazingira yetu tuliyonayo. Kwa kweli bado mazingira yetu hayajafikia *standard* na wala hatuwezi tukajisifu au kujivunia kwamba Unguja pamoja na Pemba tumefikia kwenye kiwango kizuri cha afya ya jamii.

Kwa hivyo, hapa katika wizara hii ina kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba utendaji wa shughuli zake wizara zinaendeshwa na hawa maafisa ambao wizara imewachagua.

Mhe. Spika, ninachomuomba Mhe. Waziri baada ya mswada huu kupita kwa kuwa wao wako tayari kutekeleza haya, basi lazima wizara ijipange vizuri sana kiutendaji. Kwa mfano, hapa tumeambiwa watakuwepo maafisa wa afya ya jamii na mazingira.

Vile vile nataka nijue kutoka kwa Mhe. Waziri kwamba hii hali ambayo inayozungumzwa katika mswada huu haikuainishwa maeneo, isipokuwa imezungumzwa kijumlajumla. Mhe. Spika, nataka nimuulize Mhe. Waziri kwamba amekusudia katika kuweka usafi na umuhimu wa mazingira katika eneo lote la Unguja na Pemba kila mahala au amekusudia mahala maalum.

Kwa ninavyofahamu mimi ni kwamba lazima Mhe. Waziri ajikite katika mambo haya kwenye sehemu za vijiji, wilaya na mikoa na wala isiwe masuala haya yanaangaliwa hapa mjini tu, na hapo bado mswada huu itakuwa haujatekelezwa unavyotakiwa.

Mhe. Spika, ninavyoamini kama ikiwa wizara imejikita kwenye masuala ya usafi wa mazingira ya jamii, basi lazima ihakikishe kuanzia kijiji, wilaya pamoja na mkoa wake mzima, na kama hali itakuwa hiyo basi mimi naungana naye vizuri, lakini labda pengine anaweza kusema kwamba aa! Tutakwenda hatua kwa hatua kwanza tutanza mjini na baadaye tutakwenda mashamba. Kwa kweli haya yanayozungumzwa humo katika mswada huu hayako mjini tu hata kwenye maeneo ya mazingira ya mashamba yako haya.

Mhe. Spika, suala muhimu kwa hawa maafisa ambao watakaojipanga katika kazi ni suala zima la kutoa huduma na utoaji wa huduma itategemea kwanza huyu aliyeajiriwa kuifanya hii kazi. Je, hii kazi ataifanya kwa uadilifu, kwa sababu si hoja kumwambia wewe utakuwa Afisa wa Mazingira, lakini baada ya kuwa yeye amepewa kile cheo kuwa aifanye ile kazi, basi haya tunayoyazungumza ambayo yametajwa ndani ya huu mswada yako vile vile. Kwa maana hiyo, itakuwa hii dhamana ambayo amepewa huyu afisa itakuwa haina maana.

Sasa mimi nataka kusema tu kwamba, pamoja na hayo yote kuwa maafisa hao watakuwepo, lakini tunaamini haya yapo na nitayataja moja baada ya jengine kama yalivyotajwa ndani ya mswada.

Kwa kweli mara nyingi tunapokuwa tunazunguka hapa mjini bila ya kwenda mbali sana, tunaona hali ya mazingira machafu. Kwa mfano, karo zimejaa na baadhi ya wakati zinafurika na maji machafu yanatoka nje ya karo, na hiyo itakuwa tayari ni dhamana ya afisa wa mazingira kuweka hali ya mazingira yale ya jamii katika hali ya usafi.

Maji machafu yanayomwagwa, ambapo wakati mwengine watu wako kwenye nyumba za ghorofa na mtu anapita anamwagiwa maji ya kichwa, hayo yapo maji machafu ambayo yanamwagwa nje ya mazingira. Pia takataka zimezagaa katika mji wa Unguja kila pahala unapokwenda. Sasa hapa mimi naona wizara ina kazi kubwa sana kuhakikisha jinsi gani mazingira yetu yataweza kuwekwa katika hali ya usafi.

Kwanza mimi nahisi pamoja na kuwa wizara itachukua hatua hii ya kuhakikisha kwamba usafi unaendelezwa, hili suala si la wizara peke yake, hili suala ni letu pamoja. Wananchi tunaoishi katika majumba ni lazima sisi wenyewe kukubali kuweka usafi na tukatae uchafu kama tunavyokataa malaria. Kama tutakataa uchafu sisi wenyewe basi mimi naamini kwamba mazingira yatakuwa safi.

Sisi ambao tunaishi kwenye mazingira haya hatujathamini nini usafi, basi mambo haya yataendelea pamoja na kuwa maafisa wapo, pamoja na kuweka sheria kali kali za kuwadhibiti hawa hiyo yote haitosaidia. *Unless and until* kwamba sisi wenyewe tuko tayari kuweka mazingira yetu ya ndani na mazingira yetu ya nje yawe safi, sisi wenyewe.

Mimi naamini hiyo ni kazi kubwa, sasa tufanye nini Mhe. Waziri? Mhe. Waziri una kazi kwanza ya kuwaelimisha watu kwenye hili suala zima, kwamba tunahitaji kumuona kila mtu ashiriki katika usafi wa mazingira yake ya ndani na mazingira ya nje. Si vyema mtu kukaa kwenye dirisha akatupa taka nje, ule sio ustaarabu. Tunasema Zanzibar tangu karne na karne, ustaarabu uko Zanzibar. Nchi zote hizo wameiga ustaarabu kutoka Zanzibar. Inakuwaje leo hali ya Zanzibar mazingira yake ni machafu kiasi hichi, wakati suala hili tunalipigia kelele kila siku.

Mimi nafikiri Mhe. Waziri ana kazi, si hoja kuzungumza katika Baraza, si hoja kuweka makabrasha ndani ya makabati. Cha msingi ni kuhakikisha kwamba kile alichokipanga waziri kinatekelezwa. Kwa hivyo vipi tutazishughulikia karo zetu, vipi tutashughulikia maji machafu, vipi tutashughulikia taka taka ambazo tunazitupa sisi wenyewe nje ya mazingira.

Mhe. Spika, katika nchi zilizokuwa zimeendelea tunakuta kila nyumba taka zake za ndani anaekewa mfuko wa *plastic* mkubwa anaweka nje. Taka za ndani zinatiwa katika mfuko wa *plastic*, asubuhi mapema hakuna ruhusa ya kutupa mtu taka nje. Taka zile unazidhibiti wewe mwenyewe unazitia ndani ya mfuko wa *palastic*. Asubuhi na mapema gari linapita linachukua mfuko ule wa *plastic* wa taka.

Watu walioajiriwa wanahakikisha wale watu wanaokota taka taka za ndani ya mji. Sasa haya yote sijui kama yatafanywa, hilo kwa wenzetu walioendelea. Tuseme huko ni mbali hatuna labda uwezo huo, lakini tuwaelimishe watu wetu wahakikishe kwamba hizi kero ndogo ndogo tunaziondosha.

Mhe. Spika, kuna mambo mawili. Kuna mambo mengine ambayo sisi wenyewe tunayasababisha. Katika majumba yetu tunayoishi wamo panya wengi sana, mende wamejaa ndani ya majumba, vidudu vyengine vimo ndani ya majumba vinatoka chini vinapanda ndani ya majumba au vinaingia ndani ya majumba. Ni silaha gani ambayo huyu waziri atampa uwezo huyo Afisa wa Wilaya au wa Mkoa au wa Kijiji kuweza kuonana na watu wanaoishi ndani ya nyumba kuwasikiliza angalau matatizo waliyonayo ndani ya nyumba zao. Hili ni suala la msingi sana.

Unajua saa nyengine mtu fulani anapokuwa na maradhi anaweza kuwa yeye mwenyewe hajifahamu kwamba yeye anahitajika kwenda hospitali ili apate matibabu. Lakini pengine jirani yake anaweza akamwambia bwana wee kwa hali hiyo uliyonayo wewe unaumwa nenda hospitali ukatafuta matibabu.

Mimi ninachokiamini katika maelezo haya ni kwamba huyu Afisa asiwe ni Afisa wa kuangalia mazingira ya nje tu, lakini huyu Afisa awe na uwezo, awe na mamlaka ya kuweza kupita katika kila eneo lake alilowekewa, akaonana na watu waliokuwemo ndani ya nyumba, asikilize matatizo waliyonayo ili yule aliyepewa dhamana ile aweze kuwasaidia, kama ni dawa za kuuza panga au kama ni chochote aweze kusaidia. Hapa nafikiri tukifanya mashirikiano baina ya Afisa aliyeteuliwa nafikiri mambo haya yataweza kuondoka.

Ndani ya mji wa Zanzibar tunaamini sote mapanya yamejaa tele humu yanakwenda tunapigana nao vikumbo pamoja na paka waliomo ndani ya majumba bado wanashindwa kuwakamata mapanya na mende waliokuwemo ndani ya nyumba. Hili nataka niseme kwamba hawa panya na hawa mende yanasababishwa na urundikaji wa vitu ambavyo havina umuhimu ndani ya nyumba. Ndani ya nyumba ya mtu inawezekana kuna magorojo na mambo kadha wa kadhaa hayakupangwa kwa utaratibu mzuri. Inawezekana nyumba ile ikawa wanahamia mapanya ndani ya nyumba ile. Kwa sababu mazingira ya ndani ya nyumba ni machafu. Kwa hiyo kama ndani ya mazingira ya nyumba hayapo safi uwezekano wa kufuga madudu kama hayo yatakuwepo.

Mhe. Spika, ndio maana nilipomtaka waziri kwamba huyu Afisa atakaeteuliwa si kwa kuangalia mazingira ya nje tu, vile vile aweze kupita nyumba kwa nyumba kusikiliza matatizo waliyonayo watu. Watu wengine hawawezi kusema wanaogopa matatizo yao. Tukifanya hivi nafikiri itatusaidia.

Jambo jengine kuna suala ambalo limezungumzwa ndani ya Mswada huu wadudu waharibifu, hili ni suala muhimu. Wadudu waharibifu tuwataje hao hao panya na mende, wanakiharibu chakula kile, wanatia uchafu ndani ya chakula. Panya wana maradhi ya *plague* ni maradhi mabaya sana kwa binaadamu. Lakini binaadamu pengine aliyekuwemo ndani hajui kama panya ana maradhi ya *plague*, hajui kama mende ni mmoja anasababisha kuchukua uchafu na kuutia pahala. Masuala haya ni muhimu sana, yanatakiwa yafanyiwe kazi. Wadudu waharibifuu wapo kwa wingi na kama tunataka tufanye hivi ni lazima tumpe mikakati na maelezo mazuri huyo Afisa atakayehusika, sio kumwambia tu nenda ukafanye kazi mahali fulani ukasimamie.

Mhe. Spika, mimi nataka nimpe Mhe. Waziri, katika hawa maafisa ambao watakaochaguliwa kusimamia hizi kazi. Nilitaka hawa maafisa wapewe uniform maalum wasuvae nguo za kawaida, hizo hazitosaidia. Kwa sababu yule hatotambulikana wala watu hawatomkubali. Lakini kama yule Afisa atakuwa na kivazi maalum, atakuwa na kibali kinachoonesha kwamba yeye ni Afisi ambaye anaangalia mazingira ili watu wamuelewe kwamba huyu ni Afisi Mazingi anaesimamia uchafu wa mazingira wa ndani na nje.

Ningelimuomba Mhe. Waziri kwamba hili suala nalo alifikirie kwamba hao watu watakaopeleka pamoja na afisa wake akikubali na hayo kwamba na yeye na nguo maalum ili watu wamtambue hilo litakuwa ni suala muhimu.

Jengine ambalo Mhe. Spika, nataka nilizungumze katika huu usafi wa mazingira kuna sehemu kadha wakadhaa. Kuna vyakula ambavyo vyengine vipo nje ya mazingira na kuna vyakula vyengine vipo ndani ya mazingira. Nje ya mazingira ni vile vyekula ambavyo watu wanaviweka nje kuuza yaani ni biashara ndogo ndogo. Biashara hizi najua hapo kale tulikuwa tunatumia jina la *Health Inspector* hawa wanapita kuangalia mazingira na anakuwa na nguo zake maalum anajulikana kwamba Afisi mazingira sasa kaingia.

Kama masuala haya hayafanywi itakuwa ni matatizo Mheshimiwa. Biashara ndogo ndogo zimejaa mji mzima, mama ntilie yuko, vyakule vinauzwa, haijulikani afya ya jamii pale inahifadhiwa namna gani katika mazingira yetu. Kama huyu mtu ambaye hana elimu ya kutosha juu ya masuala atazungumza nini. Lazima Mhe. Waziri umchague mtu ambaye ana elimu ya kutosha katika masuala haya. Awape elimu watu hawa, ubaya wa kuwa vyakula vyao hawavifuniki. Zamani ilikuwa huwezi kukuta chakula nje kimewekwa wazi. Ukipita katika maeneo utakuta maandazi hayakufunikwa, visheti havikufunikwa, pengine anauzwa vyakula vidogo vidogo viko wazi.

Tunajua kuwa adui inzi yupo na ni mbaya ambaye akitua, yule ni *carrier*, ile miguu yake inabeba vitu vichafu, miguu yake ina kama nta anatoa kamka mbu wa malaria. Mbu wa malaria kabla hajakutafuna kawaida yake anamimina. Baada ya kumimina sasa yeye nachukua, hiyo ndiyo kawaida yake mbu. Utasikia mara tayari malaria, kachukua huko kakumiminia wewe halafu ile yako safi yeye ndio anachukua.

Kwa hivyo na huyu nzi ni *carrier* wa maradhi, vyakula vilivyokuwa vimewachwa hazi havikutiwa katika kabati la kiyoo uwezekano wa watu kupata maradhi yule anasababisha tumbo la kuharisha. Hivi vyakula tunavyoviona katika mazingira ya nje, tunapita tunaona lakini hatuna uwezo wa kusema. Lakini pengine ikijakuwa tayari hii sheria na sisi Wawakilishi wa majimbo tunayo nafasi ya kuzungumza katika majimbo yetu kuweka hali ya mazingira ya usafi pamoja na vyakula kumsaidia huyu afsa. Huo wote ni uchafu, kwa hivyo hawa maafisa wawe na uwezo wa kuhakikisha kwamba mazingira ya vyakula vinavyowekwa nje vipo katika hali ya usafi.

Jambo jengine Mhe. Spika, katika suala la afya safi ya jamii, kuna mambo ambayo yanajitokeza watu wanahitaji kupata kinga za afya ya jamii. Hili ni suala muhimu sana watu kupata kinga za afya ya jamii. Nani atakuwa

dhamana wa kinga ya afya ya jamii? Ni hawa maafisa ambao watahakikisha usafi na usalama wa wananchi kwamba watu hawa litakapotokezea jambo la *emergence* ya maradhi fulani yameingia basi huyu Afisa atakuwa ni dhamana kuwaambia watu kwamba jamani kuna kitu kadhaa na mnatakiwa mkachome sindano au mnatakiwa mkale dawa au vyenginevyo.

Afisa wa Kinga ya afya ni mtu muhimu vile vile. Huyu sijui kama atachaguliwa na wengine au mwenyewe waziri ndio atapanga, sijui atapanga vipi kwa sababu sote tunaumwa huko, tukiwa mashamba, tukiwa mjini tunaumwa kila wakati na hatujui tunadhuriwa na kitu gani. Baada ya mgonjwa kwenda hospitali na kuchunguzwa madaktari wanajua kwamba katika mtaa fulani kumeshatokezea maradhi fulani. Kwa hivyo inavyotokezea inabidi ni lazima amueleze afisa wake na yeye inabidi achukue hatua.

Ndio pale niliposema kwamba huyu Afisa asiwe wa kuangalia mazingira ya nje tu hata mambo yanayotokezea ndani ya majumba na yeye awe na uwezo wa kuweza kuonana na watu wa ndani ya nyumba. Taarifa ni kitu muhimu na taaluma ni kitu mihumu. Huyu Afisa akiwa wa Wilaya akiwa ni wa Mkoa ikiwa ni wa kijiji anawajibu kuwaita watu wake kuwapa elimu juu ya suala hili. Hapo nafikiri tukifanya jitihada ya pamoja sote Wawakilishi mafisa na viongozi mbali mbali naamini mazingira haya yatakuwa safi. Lakini bila ya kuwa na mashirikiano ya pahala pamoja ikawa sisi mzigo huu tunamtupia mtu mmoja, hakuna kazi inayofanywa na mtu mmoja ni ushirikiano wa pamoja ndio jambo linakuwa. Mhe. Waziri mimi ningekuomba hili suala ukaliangalia kwa kina, huu Mswada ni mzuri na unafaida kwetu na tunaupenda, lakini una kazi kubwa sana.

Mhe. Waziri nilitaka kusema kwamba huduma siku zote inatakiwa iwe nzuri, hatupendi sisi kuona kwamba afisa aliyechaguliwa anashindwa kutoa huduma katika kijiji. Tukibaini mimi kama ni Mwakilishi wa jimbo na najua kwamba mtu fulani kapewa dhamana na kafanya dharau ya hali ya juu. Mimi kama ni Mwakilishi siwezi nikamuachilia lazima nitamwambia kwamba wewe bwana Afisa umechaguliwa, uchafu namna kama hii, mataka yamejaa namna kama hii, makaro yanafurika, unafanya nini hapa. Ni lazima nimwambie kwa sababu na mimi nina nafasi yangu kama ni Mwakilishi wa jimbo, kuona katika eneo langu linakuwa safi kwa sababu na mimi napenda usafi.

Mhe. Spika, hapa mimi nafikiri ni suala muhimu kwamba huu usimamizi uwe mzuri na kama yeye anapewa cheo hichi hakufanya kazi. Sisi tuna nafasi ya kumripoti Afisa huyo kwamba hafanyi kazi zake vizuri. Eneo lolote au Afisa yoyote atakaeteuliwa hakufanya kazi zake vizuri wananchi wamripoti haraka iwezekanavyo kwa sababu hafanyi kazi zake sawa sawa. Hapo tutapata usafi na afya zetu zitakuwa nzuri na afya ya jamii kwa jumla itakuwa nzuri.

Mhe. Spika, hakuna kitu muhimu kama mtu kuwa muadilifu katika kazi zako. Tunaomba watu watakaoteuliwa wawe waadilifu katika kazi zao na wawe waaminifu. Hii nchi inanuka harufu ya rushwa ndani ya Zanzibar na ipo bado haijaondoka. Sasa mtu akipenyezewa kitu anamuachia aendelee na uchafu wake, kitu hichi sio kizuri. Lazima tuwe waadilifu na tuwe waaminifu katika kazi zetu ambazo tunateuliwa. Hili namueleza Mhe. Waziri aweze kulifahamu. Huyu lazima afundishwe nini miko ya kazi, huyu afisa lazima apewe miko ya kazi, asiachiliwe tu akatoka kama bumbla, apewe vitu vya kutosha, eneo lolote atakaloulizwa la kisheria ya afya aweze kujua na kuweza kulitekeleza.

Mhe. Spika, Mswada huu una sheria ambazo sheria hizi tunazitaka sisi tuzifuate. Lakini haitakuwa vyema ndani ya sheria ya Mswada huu kuweza tu mtu kwa sababu yeye Afisa na sheria ipo, ukamchukulia mtu hatua, hilo litakuwa ni kosa kubwa sana hilo. Hata sisi tunapokuwa maafisa tunapewa dhamana katika mawizara yetu serikalini, mfanyakazi akifanya kosa tunampa karipio, tunampa onyo, tunamwambia kiasi mara mbili au mara tatu, halafu akiwa mtu mkaidi hasikii ndio pale tunamchukulia hatua. Sheria hii ipo kweli lakini kwa sababu tuna-*deal* na *public administration* kwa hivyo ni lazima sisi pahala petu huona kwamba watu hawa wanaeleweshwa masuala haya na sio kumvamia tu, kwa sababu sheria ipo unamwambia kwamba leo nakushtaki na nakupeleka mahakamani.

Mimi ningeshauri kwamba hao watu wawe wastahamilivu, wawe na *policy* na namna ya ku-*deal* na jamii, wawe watu madhubuti, hata tena ikifika hadi kumchukulia mtu hatua za kisheria inajulikana kwamba huyu mtu sugu, hakuna tena jengine ila ni kumchukulia hatua tu, hapo tena hatakuwa na kosa huyo Afisa kuchukua hatua hiyo. Lakini si kwa sababu ya sheria kwa kuwa tu mara ya mwanzo sheria kwamba ipo ndio akachukuliwa hatua. Hapa kuna sheria kali sana, ikiwa mtu hakufanya hivi na hivi kuna adhabu na kuna faini kubwa.

Jambo jengine Mhe. Spika, katika zunguuka zunguka yake huyu Afisa ambae atachukuliwa kuangalia afya ya jamii na matatizo yoyote yanayojitokeza, lazima huyu Afisa papatikane *coordination* baina ya yeye Afisa ya mkubwa wake wa kazi. Si vyema akenda huko katika kazi zake kaona mambo kadha wa kadha akawa yeye yale mambo hakuyatoa kwa mkubwa wake, hilo litakuwa ni dhambi na itakuwa ni kosa kubwa sana. Huyu afsa atakapoona jambo limejitokeza katika maeneo ni mahala pake afisa huyu kuweza kuyapeleka kwa mkubwa wake. Ni lazima apeleke na ni lazima waziri umuulize wakati wanapofanya vikao vya kila wiki, umuulize ehee Afisa wangu wewe una nini, wewe umepata nini, wewe umekuta nini. Sasa pale wanapokaa maafisa na waziri wake wanasema mimi nimekuta na jipya hili, hili na hili. Nafikiri kwa njia hii, kazi inaweza kuwa nzuri. Lakini bila ya hizi taratibu ambazo nilizozizungumza itakuwa hii sheria makabrasha haya yatatiwa ndani ya kabati na huyu Afisa mambo yake atayatia ndani ya kabati, atakwenda yeye kama ni Afisa na uwezo wake basi, hafanyi chochote na hapa hapa tutayaona. Wakati Mswada utakapokuwa unakwenda na umemalizikia basi tutaona baadae.

Mhe. Spika, jambo jengile la msingi na la mwisho ni lazima aweze kutoa elimu juu ya suala hili. Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nitumie ibara ya 72 inayozungumzia kiwango cha vikao 72(1) na 72(2). Naomba kwa heshima na taadhima Mhe. Spika, uniruhusu ninukuu.

Ibara ya 72(1) "Kiwango cha vikao vyote vya baraza kitakuwa ni nusu ya Wajumbe"

(2) Mara kabla ya uamuzi wowote kufanyika, ikiwa mjumbe yeyote aliyehudhuria atapinga kwa kudai kwamba mbali na Spika, wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote basi kama Spika atathibitisha kuwa wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya wajumbe wote atasimamisha shughuli kwa muda wa dakika tano na huku muhudumu kwa maelekezo ya katibu akipiga kengele kwa vituo yaani sio mfululizo."

Kwa kuwa Kanuni hii imeshahojiwa mapema na ukaamuru kwamba papigwe kengele na karibu tumeshatumia karibu nusu saa nzima tunasubiri wenzetu na koram bado ni ndogo. Inaonekana wenzetu wa Chama cha Mapinduzi *back benchers* wana *party caucus.* Nadhani ungetupa maelekezo kama ni kuakhirisha kikao mpaka wamalize wenzetu ili tuendelee na mijadala. Lakini sasa mijadala iko ukingoni na wenzetu mpaka sasa hivi hakuna dalili ya kutokea na tunataka kupitisha maamuzi mazito ya kuwathibitisha hawa wasimamizi na wasaidizi wasimamizi wa afya ya jamii na mazingira.

Sasa nadhani ingekuwa vyema Mhe. Spika, tukaahirisha kikao mpaka wenzetu Chama cha Mapinduzi *back benchers* wakamaliza *party caucus*, kusudi baadae tuendelee.

Mhe. Spika: Mhe. Saleh Nassor Juma, mjadala haujaisha, kuna wachangiaji wanaendelea. Kwa hiyo tuendelee na uchangiaji tutaona hapo baada ya kumaliza mchango wa waheshimiwa waliobakia.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuchangia kidogo tu kwenye Mswada huu mkubwa na wenye madhumuni makubwa.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mchana huu kuwepo hapa katika kazi zetu za kawaida za Baraza. Pili nikushukuru wewe kwa busara zako za kuliongoza hili Baraza letu.

Mhe. Spika, siku moja wakati tunamuaga mwalimu wetu wa darasa tunamuaga anarudi kwao Ujerumani alisimama na akasema maneno haya.

"Ana bika tele la furaha na anafumbato tu ya masikitiko"

Alisema ana furaha kwa sababu anarudi kwao na alikuwa ana masikitiko kwa sababu anaondoka na kwa kuwa tumezoeana. Alisema msemo huu na mimi nitausema msemo huu lakini kwa kinyume chake. Mimi nna bika la masikitiko na fumbato ya furaha. Nna masikitiko makubwa juu ya Baraza lako la leo.

Toka mimi nijuunge miaka miwili iliyopita sijaliona likiwa linaendelea hivi isipokuwa leo. Hili linanisikitisha tena sana. Mimi nilikuwa nikuandikie kinoti cha kuondoka, lakini nilipoona hali hii hata kwenda haja ya kujisaidia naona tabu kutoka kwa hali ya ukumbi ulivyo.

Furaha yangu ndogo ni kwamba ukiwa kama waziri na *backbencher* moja tu, kwa vile watu wote waliobaki ni watu wa aina yangu, ukiwacha mawaziri kuna *backbencher* moja tu, wengine wote ni mawaziri, hii ndio furaha yangu ndogo. Hii Mhe. Spika, inaonesha kwamba sisi au mimi na wenzangu wa aina yangu baada ya maelekezo yako ya wiki iliyopita tulikufahamu, tulikuelewa na tutaendelea kutii Kanuni, Sheria na Misingi ya Baraza kama ilivyo. Pale mtu akiondoka itakuwa tunaudhuru wa kilazima, sisemi kuwa wengine hawana lakini Baraza kuwa katika hali hii kwa kweli ni hali ambayo mimi haikunipa faraja hata kidogo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, Mswada huu unaozungumzia usajili na usimamizi wa maafisa wa afya ya jamii na mazingira ni mzuri na umekuja katika wakati wake. Mazingira yaliyotuzunguka Zanzibar yanahatarisha amani ya afya zetu, si vijijini wala sio mjini. Kwa kweli afya zetu au hali ya mazingira yanayotuzunguuka si nzuri. Ipo haja Mswada huu baada ya kupita na kuwa sheria, hiyo sheria baada ya Mhe. Rais kuithibitisha iweze kuanza kazi mara moja na kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa.

Mswada huu pindipo ukipita kuwa sheria, hao Maafisa ambao wanatajwa kuwa Maafisa wa afya sijui watu hawa ni kama wale ambao zamani tulikuwa tunawaita RHA au ni watu wa aina nyengine. Lakini kwa kuwa hawa walikuwa wakifanya kazi katika maeneo mbali mbali lazima wawe na vitambulisho vya kufanya kazi yao na wizara iwaelimishe namna ya kwenda katika jamii.

Kazi yao ni kusimamia afya inahitaji maelekezo, kwa hiyo wawe watu wenye hekima na busara ambao watu watawakubali kuwatumikia, wasiwe watu wenye dua kali inayotisha. Ni vyema baada ya kusajiliwa na kupata leseni ya kufanya kazi pia waandaliwe vitambulisho maalum ili ajulikane huyu ni afisa wa aina fulani anayetupitia katika mazingira yetu.

Mhe. Spika, katika Mswada huu kumetajwa kuwa lile Baraza litamteua mmoja wao miongoni mwao kuwa Makamo Mwenyekiti, kundi haliwezi likateua nadhani kama ni kwa makosa au vipi. Kundi linaweza likachagua, nadhani pale ingekuwa Baraza litamchagua mmoja wao kuwa Makamo Mwenyekiti badala ya kuteua. Ingelikuwa anateua Raisi, Waziri mwenyewe au mwenyekiti wa Baraza, ingekuwa ni kuteua, lakini kundi haliwezi likateua.
Mhe. Spika, mimi nimesimama kwa kutoa maoni yangu machache. Baada ya hayo naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

Mhe. Farida Amour Moh'd: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia machache sana katika Mswada huu muhimu. Kwanza naomba nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake. Nimpongeze sana kwa kuletwa Mswada huu muhimu katika mda huu tulionao.

Mhe. Spika, afya ya jamii ni muhimu katika nchi yeyote ile duniani. Katika hili nasema nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea Mswada huu. Mswada huu ni muendelezo wa Mswada uliopita juzi ni katika kuyatilia mkazo ili Mswada huu upate kuwa sheria na ufanye kazi vizuri ndani ya jamii zetu.

Mhe. Spika, mimi naomba nimwambie Mhe. Waziri, nina imani sana na mabaraza haya katika undwaji wa mabaraza kama yatafanya kazi. Kwa uwadilifu mkubwa katika taasisi zetu au katika jamii yetu, lakini kitu kizito kidogo ni kufanyakazi na jamii. Kwa sababu ndani ya jamii yetu kila mmoja ana tabia yake, kila mmoja ana maumbile yake Mwenyezi Mungu aliyomjaalia.

Namuomba Mhe. Waziri hatuna tatizo na Mswada huu, Mswada huu ni mzuri, tumeuelewa, tumeufahamu vizuri na tunauhitaji tuupitishe. Naomba Mhe. Waziri baada tu ya kupitishwa Mswada huu na kuundwa kwa mabaraza haya afanye jambo muhimu sana. Aandae mafunzo maalum kwa wale maafisa wenye Baraza halafu na mafunzo hayo pia yaandaliwe kwa jamii ili jamii ijue wajibu wake jinsi ya kukaa na wale maafisa wa Baraza. Baraza nalo pia lijue wajibu wake jinsi ya kuishi na ile jamii watakayofanya nayo kazi. Hili ni muhimu Mhe. Spika, kwa sababu bila ya mafunzo huwezi kufanya kitu chochote kile. Wapewe elimu nzuri wajue nini cha kufanya na vipi vya vya kukaa. Wale na wao watoe elimu nzuri kwa jamii inayotaka kufanya nao kazi.
Mhe. Spika, pia kuna kipengele kimoja kimeelezea uwezo wa waziri kutunga kanuni. Baada ya kumalizika hili baada ya kupitishwa Mswada na kuwa sheria. Nakuomba Mhe. Waziri usilicheleweshe hili la kutungwa Kanuni ili

tupate maendeleo mazuri katika kukaa na jamii yetu na kufanya jambo tulilolikusudia. Baada ya hapo naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe nafikiri yale maombi mengi yaliyokuja ili tuakhirishe kikao wakati wake sasa ndio huu. Mhe. Waziri pamoja na naibu Waziri wapate nafasi jioni na pia kunamasuala muhimu sana ambayo Mwanasheria Mkuu atatusaidia katika kuuweka vizuri Mswada huu. Kazi hiyo nayo ifanyike jioni.

Kwa maana hiyo basi tusitishe shughuli zetu hadi jioni ili kuwapa nafasi Mhe. Naibu Waziri na Waziri wake na Mhe. Mwanasheria Mkuu wakishirikiana na Wizara kuweka mambo hayo ya Mswada huu kukaa vizuri zaidi na jioni hiyo tuweze kupitisha.

Ila nataka niseme jambo moja, koram imetupa shida kidogo, nashukuru kwamba uchangiaji umeendelea mpaka kipindi hichi lakini shughuli zetu zimekuwa ni nyingi mno. Lakini pia tuelewe na shughuli hii nayo ndiyo shughuli hasa ambayo ipo kwenye mtitiriko wa kikao hichi.

Kwa hiyo niombe kwamba jioni sisi tuliokuwepo na wengine ambao hawapo tupeane taarifa tufike kwa wakati ili tumalize shughuli hii. Sio kazi kubwa sana iliyobaki, kwani mtitiriko wa michango inavyoonekana mambo yote yapo *all most positive* isipokuwa kuhitaji maelekezo na ufafanuzi wa hapa na pale kwa baadhi ya hoja ambazo waheshimiwa wajumbe wameuliza. Kubwa zaidi na lenye umuhimu ambalo Mhe. Mwanasheria Mkuu na yeye pia atatusaidia wakati wa jioni. Tuhimizane tutimieze wajibu wetu katika kufanya shughuli zetu hizi. Nakuombeni sana Waheshimiwa wajumbe.

Baada ya machache hayo tuakhirishe kikao hichi hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 6.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hali iliyomo ndani ya ukumbi wangu huu hainivutii kama shughuli za kikao zinaweza zikaenda hivi sasa na muelekeo hapo nje wa kuona Wajumbe gani labda wamejikusanya kusanya ili kuingia ndani nao pia hainipi faraja. Kwa sababu kimsingi hakuna Wajumbe. Muelekeo huu unatwambia kwamba shughuli hii inabidi tuisitishe kwa leo na moja kwa moja tuite kesho asubuhi ili tupate nafasi ya Waheshimiwa Wajumbe sote kutafakari juu ya hali halisi tuliyonayo, lakini pia na fadhaa ambayo wananchi wetu imewapata isiyotegemewa na isiyokuwa ya kawaida huko nje, kidogo kuna fadhaa. Taarifa niliyonayo ni kwamba njia nyingi zimefungwa na kidogo hali hiyo imewasababisha baadhi ya Wajumbe wangu wasipate wasaa wa saa hizi kufika hapa kwa urahisi.

Kwa hivyo nichukue nafasi hii kupitia kwenu Waheshimiwa Wajumbe mliopo na kumshukuru sana Mhe. Waziri anayasikia haya. Tutoe nafasi basi tusifanye shughuli hii tukaimaliza katika hali ya kufadhaika fadhaika, tunatakiwa tufanye mambo yetu tukiwa tumetulia, tunakwenda vizuri, ili tufanye kitu kwa ufanisi ulio mkubwa.

Nichukue nafasi hii basi kuwashukuru Wajumbe mliopo pamoja na Makamo wa Pili wa Rais.

Sasa naakhirisha kikao hiki hadi kesho saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 11.05 jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 19/10/2012 saa 3.00 asubuhi)